Basi Macho Yao Yalipofumbuliwa, Walimtambua

Na kutoka katika Injili ya Luka Mtakatifu, kuanzia mlango wa 24 na kifungu cha 13.

Na tazama, siku ile ile watu wawili miongoni mwao walikuwa wakienda kijiji kimoja, jina lake Emau, kilichokuwa mbali na Yerusalemu kama mwendo *wa saa mbili.*

Nao walikuwa wakizungumza wao kwa wao habari za mambo hayo yote yaliyotukia.

Ikawa katika kuzungumza na kuulizana kwao, Yesu mwenyewe alikaribia, akaandamana nao.

Macho yao yakafumbwa wasimtambue.

Akawaambia, Ni maneno gani haya mnayosemezana hivi mnapotembea na kukunja nyuso zenu?

Akajibu mmoja wao, jina lake Kleopa, akamwambia, Je! Wewe peke yako u mgeni katika Yerusalemu, hata huyajui yaliyotukia humo siku hizi?

Akawauliza, Mambo gani? Wakamwambia, Mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote;

Tena jinsi wakuu wa makuhani na wakubwa wetu walivyomtia katika hukumu ya ninii. . .ya kufa, wakamsulibisha.

Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya haya yote, leo ni siku ya tatu tangu yalipotendeka mambo hayo;

Tena wanawake kadha wa kadha wa kwetu walitushitusha, waliokwenda kaburini asubuhi na mapema,

Wasiuone mwili wake; wakaja wakasema ya kwamba wametokewa na malaika waliosema. . .yu hai.

Na wengine waliokuwa pamoja nasi walikwenda kaburini wakaona vivyo hivyo kama. . .wanawake walivyosema, ila yeye hawakumwona.

Akawaambia, Enyi msiofahamu,. . .wenye mioyo mizito ya kuamini yote waliyoyasema manabii!

Je! Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na akaingia *katika utukufu wake?*

Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza…maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe.

Wakakikaribia kile kijiji ambacho *walikuwa wakienda, naye alifanya kama anataka kuendelea mbele.*

Wakamshawishi wakisema, Kaa pamoja nasi, kwa kuwa kunaelekea *kuchwa, na mchana umekwisha. Akaingia ndani kukaa nao.*

Ikawa walipokuwa *wameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa.*

Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao.

Wakaambiana, Je! Mioyo *yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi, na kutufunulia* sisi maandiko?

2 Na tuombe, tuinamishe vichwa vyetu sasa katika maombi.

3 Mungu Mtakatifu sana, tunakukaribia katika Jina la Yesu, Mwanao. Nasi tunaamini tuko Mbele Zako sasa, kwa kuwa kwa imani tunakuja kwenye madhabahu Yako makuu Palipo na Damu Yake, inayonena kwa niaba yetu. Na kwa kweli sisi ni watu wahitaji, Bwana. Tunakuhitaji Wewe, nasi—nasi tunaomba neema Yako. Na tunapoona unabii ukitimizwa leo, kwamba ka—kanisa, jinsi ambavyo tumekuwa matajiri katika mambo ya ulimwengu, nasi tunafikiri hatuna haja ya kitu, Naye alisema sisi ni "uchi, vipofu, wenye mashaka, na vipofu, wala hatujui." Pia, Baba, tunaomba neema, basi, kwamba Wewe utayafumbua macho yetu tupate kulifahamu Neno Lako, tuweze kuifahamu saa tunayoishi, tupate kujiandaa kwa ajili ya kuonekana Kwake, kwa kuwa kweli tunaamini kumekaribia. Kwa hiyo sasa tunaomba ya kwamba ungetupatia, usiku wa leo, shauku za moyo wetu, kulingana na utajiri Wako Utukufuni.

4 Ukitusamehe dhambi zetu, Bwana. Tu—tunaomba ya kwamba hutaangalia kutokuelewa kwetu na ujinga we—wetu, kuhusu mambo tunayopaswa kujua, kwamba utatusamehe kwa hayo. Pia utukumbuke, kama wanadamu tu, Baba, sisi hufanya makosa ya kila namna mara kwa mara na matatizo. Wewe ni Mungu wa milele, asiye na kikomo, asiyeweza kukosea. Tunaomba utaturehemu na kutupa baraka tunazoomba, kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

5 Sasa, tunashukuru tena usiku wa leo kwa ajili ya fursa ya kuwa hapa katika ninii…jumba hili la mikutano, na kuwa na wakati huu mzuri sana kushiriki tena kwenye mambo ya Mungu.

6 Ninasikitika kwa kuwacheleweshа jana usiku, kinyume na ahadi yangu, kwamba, niliwaambia tungetoka kila jioni kati—kati ya saa tatu na saa tatu u nusu. Na—na—nami nilichelewa jana jioni, basi—basi nasikitika nilifanya hivyo. Sasa, usiku wa leo, nitajaribu kuukomboa huo, pamoja nanyi, kwa sababu ninajua wengi wenu hufanya kazi. Na hamna budi kwenda kazini. Ninyi, ninyi watu, ninyi wanawake hamna budi kuwaandaa wanaume wenu waende kazini, na kadhalika. Pia wengi wenu hufanya kazi, na ni vigumu.

7 Nami nafikiri ya kwamba, leo hii, tumekuwa na kuhubiri kwingi. Wahudumu wengi wazuri, wahudumu hodari, ambao wametuletea Neno, wachungaji wenu na—na wainjilisti, na kadhalika, wanaopitia mjini. Lakini, nafikiri, jambo muhimu ninalojaribu ku—kujaribu kuwaletea, ni u—uhalisi wa Uwepo wa Kristo, ili—ili mweze kumwona na kujua ya kwamba Ndiye, kwa ahadi Yake iliyotambulishwa kwa ajili ya siku hii.

8 Sasa, jana jioni tulijaribu kutoa muhtasari mdogo, na usiku wa leo tuna muhtasari mwingine mdogo, na labda kesho usiku.

9 Halafu, Bwana akipenda, Jumamosi usiku, maana haitawabidi kuamka mapema sana Jumapili asubuhi, na—nataka kujaribu kuleta Ujumbe katika—katika njia ambayo ingeeleweka zaidi na wachungaji na wale wawezao, kuurejesha kwenye Maandiko.

10 Halafu, Jumapili jioni, tunataka—tunataka kufanya mstari wa ma—maombi, na kuwaombea wagonjwa, kwa kuwekea wagonjwa mikono na kuwaombea kwa njia hiyo. Nasi tuliona ya kwamba, kwa fanaka, wale wasioweza kuinuka kwa imani na kumwamini tu Yeye na kulikubali. Njia yangu ya kuliwazia, ni kwamba, ingekuwa bora kama tungeinuka tu na kumkubali.

11 Hapa Afrika Kusini, nilipokuwa kwenye mkutano kule Durban, ambako karibu watu laki mbili, nadhani, walikuwa wamekusanyika kwenye uwanja wa mashindano ya farasi wa Durban. Kulikuwako, tunaleta. . .Wana watu watano tu jukwaani. Na wakati mtu wa tano alipoponywa, jukwaani, nao hao wenyeji waliulizwa kule nje, ambako walikuwa wamekaa tu. . .Loo, jamani!

12 Vema, huo ndio mmoja wa viwanja vikubwa kuliko vyote vya mashindano ya farasi ulimwenguni. Ni mkubwa mara nyingi kuliko wa Churchill Downs, huko Louisville. Na Waingereza wote huenda kule kwa ajili ya michezo yao ya kipupwe, mbio za farasi. Nasi tulikuwa tumeuchukua uwanja huo, na wote ulikuwa umejaa kabisa, na hata kote kote ng'ambo ya uwanja huo. Nami nilikuwa ule upande mwingine, kwenye je—jengo fulani. Sidney Smith, meya wa Durban, alinipeleka kule siku hiyo, kwenye uwanja huo wa mbio za farasi.

13 Nami niliona, kwa ombi moja la kusanyiko, baada ya wenyeji hao. . . Baadhi yao hawakujua mkono wa kulia na wa kushoto ulikuwa ni upi. Nami niliwaona, wakiisha kuona . . .

14 Nami nikaelezea. Nilikuwa na wafasiri kumi na watano mbalimbali. Unaposema sentensi moja, inakubidi kungojea mpaka watu kumi na watano mbalimbali waiseme. Sasa, mnajua jinsi hilo lilivyokuwa ni gumu, kwa makabila hayo. Halafu baada ya hayo kumalizika, na kuwaelezea kifupi kwamba Yesu alikuwa ni nani. Nikasema, "Wengi wenu hapa mmebandikwa vitambulisho kama Wakristo, mngali mnabeba sanamu mkononi mwenu, hata hivyo."

15 Ndipo nikamwuliza mmoja. Nikamwambia Bw. Smith, nikasema, "Kwa nini yule mwenyeji anabeba ile sanamu? Na kama ulivyosema, 'Hicho kilikuwa ni kibandiko cha Kikristo.'"

16 Akasema, "Ndivyo." Kasema, "Yeye ni Mzulu." Kasema, "Ninaweza kuzungumza lugha yake. Hebu mwulize tu." Na kwa hiyo akafanya hivyo kwa manufaa yangu. Kwa hiyo nikaninii . . . Tukamkaribia. Nami nikamwita, "Thomas." Akasema, "Sema tu chochote, maana yeye alikuwa mwenye kushuku."

17 Nikasema, "Thomas, je! wewe ni Mkristo?" Na, ndiyo, a—aliuamini. Nikasema, "Vema, kwa nini umeshika sanamu hiyo mkononi mwako?"

18 "Vema, i—ilikuwa ni Mungu, pia. Naye baba yake aliibeba sanamu hii, ndipo simba alipomfukuza. Naye ameinyunyizia damu. Kisha—kisha akawasha moto kidogo, akakariri maombi aliyoambiwa na mchawi, nayo yakamwogopesha simba akatoroka."

19 "Vema," nikasema, "Mimi ni—ni . . . " Neno *jagter, jagter* linamaanisha "mwindaji." *Leeu, leeu jagter*, hiyo ni, "kuwinda simba." Nikasema, "Mimi ni mwi—mwindaji simba. Na si maombi hayo yaliyomwogopesha huyo simba, ilikuwa ni moto, si—simba anaogopa moto."

20 Akasema, "Vema, yeye alimwamini Amoya." *Amoya* linamaanisha ni "nguvu zisizoonekana," kama vile Mungu, ama kama upepo. Mnaona? Amoya, kitu ambacho unaweza . . . "Yeye alimwamini Amoya. Lakini kama Amoya alishindwa, *hii* haitashindwa." Mnaona? Sasa, hiyo ndiyo iliyokuwa nguvu ya Ukristo, kwao.

21 Nikawaambia. Nikasema, "Sasa, mnaona, chochote mmishenari alichowaambia kumhusu Kristo ni cha kweli. Mnaona? Lakini," nikasema, "kuna . . . Mnaona, yeye hakuwaambia yote. Alijaribu kuwaambia, kwamba, 'Nguvu Zake kuu zilikoma hapo alipokufa huko nyuma msalabani, wala hatunazo tena.' Amekosea hapo. Yeye yu hai, na papa hapa miongoni mwetu, unaona, kama tu alivyowahi kuwa."

22 Basi walipoona hilo limethibitishwa, kama vile mlivyoona jana jioni, walikadiria elfu ishirini na tano waliponywa katika wakati mmoja. Wazia hilo.

23 Halafu kesho yake, Bw. Smith akanipigia simu, na akasema, "Ndugu Branham, nenda kwenye dirisha lako, linaloelekea upande wa Bahari Hindi, chumba cha—chako cha hoteli." Ndipo yakaja malori saba makubwa mno ya Kiingereza. Loo, jamani! Hatuna lori lingaliweza kubeba theluthi moja ya kile yangebeba, zimejaa mikongojo mitupu na vibebaji, ambavyo waliwabebea wapendwa wao kutoka misituni, vimelundikwa mle ndani. Walikuwa juu yavyo, siku moja hapo kabla. Nao hawa hapa, wakitembea nyuma ya malori haya, maelfu yao, huku wameinua mikono yao, wakiimba, "Mambo yote yanawezekana. Amini tu."

24 Sasa, kama kafiri, mtu asiyejua upi mkono wake wa kulia ama wa kushoto, m—mtu aliye katika hali hiyo, anaweza tu kuona hilo likitukia wakati mmoja, ama wakati mmoja kusoma Maandiko na kumwelezea; inatupasaje sisi, ambao tunadai kuwa watu waliojazwa na Roho, tunapaswa kufanya nini? Mnaona?

25 Lakini, jambo ni kwamba, tumetiwa kasumba sana mpaka kila mtu hutoa maoni yake mwenyewe. Na, vema, ni tofauti tu na watu unaokutana nao. Unajua, kuna . . . Na kafiri kwa jumla halimaanishi inakubidi uwe asiye na elimu. Wapo makafiri walioelimika, mwajua, nao ndio walio wabaya zaidi ya wote. Hiyo, hiyo ni kweli. Unapoenda kulivuta . . . Nitawaambia. Katika kusafiri ulimwenguni, nimeuzunguka ulimwengu mara kadhaa, lakini mnajua ni wapi wanakohitaji wamishenari zaidi sana? Marekani. Papa hapa. Huu hapa uwanja wa mishenari. Hiyo ni kweli. Acheni baadhi ya hao watu waje huku, wasiojua mkono wa kuume wala wa kushoto, wakawafundishe watu hawa Mungu ni nani. Naam. Wana mambo mengi sana ya kiakili, mpaka wamepoteza mtazamo wa jambo hilo lote. Naam. Ninii tu, wanajaribu kulielelezea, na kujaribu ku—kulitatua, ama kujaribu kuliwazia.

26 Hao wenyeji hawajaribu kuwazia chochote. Yeye huamini tu kwa urahisi. Na hilo ndilo unalopaswa kufanya, kuwa sawa na Mungu, ni kuamini tu. Huwezi kumwelewa Mungu.

27 Vipi kama Musa . . . wakati alipokiona kile kichaka hakiteketei? Sasa, Musa alikuwa mkemia. Naye Musa alifundishwa katika hekima yote ya Wamisri. Bali wakati alipokiona kichaka hicho, lilikuwa ni jambo geni. Mbona, kamwe hakusema, "Sasa, ninaamini nitaenda pale. Wakati ule moto utakapozimika, nitayachuma majani kutoka kwenye kichaka kile na kuyapeleka kule chini, kwenye maabara, nione yamenyunyiziwa nini, mnaona, nione ni kwa nini kichaka hicho kingeweza kuwaka moto wala—wala hakikuteketea." Huo ungekuwa ndio mtazamo wa kisayansi.

28 Lakini alifanya nini? Alivua viatu vyake na kuketi chini na kuzungumza Nayo. Mungu akamjibu. Mnaona? Unapojinyenyekeza, jinyenyekeze.

29 Vipi kama Martha angalisema. . . aliposikia ya kwamba Yesu. . . Baada ya yeye kuitwa, aje akamwombee Lazaro, alikuwa amekufa siku nne. Vipi kama angalikimbia, aseme, "Nilifikiri tulikuwa tumeamini kitu fulani"? Alikuwa na haki ya kumkemea, mwajua, kwa kuwa Yeye alikuwa amekosa kuja hapo walipomwita.

30 Lakini, mnaona, alikuwa na mtazamo mzuri. Alimwendea, kasema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa. Na hata sasa, lolote umwombalo Mungu, Mungu atakupa." Loo! Ati nini? Jambo ndilo hilo. Wazo ndilo hilo. Mnaona? Alikuwa na mtazamo mzuri.

31 Angalia imani hiyo, wakati ilipomgusa Yesu. Alisema, "Ndugu yako ataishi tena."

32 Akasema, "Naam, Bwana. Katika siku ya mwisho, katika ufufuo wa kiama, atafufuka. Alikuwa ni mvulana mzuri."

33 Akasema, "Mimi ndimi ufufuo na uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi hatakufa kamwe. Unasadiki haya?"

34 Akasema, "Naam, Bwana. Ninaamini ya kwamba Wewe Ndiye yule Masihi, Mwana wa Mungu ajaye ulimwenguni." Loo, jamani!

"Mmemzika wapi?"

35 Nilikuwa nikizungumza na mwanamke mmoja, si muda mrefu uliopita. Nimesimulia hili, hapa jukwaani, tena. Ni watu wanaodai wanaamini uponyaji wa Kiungu; ni kuamini kiakili na kielimu, kuamini "nia kuutawala mwili." Nao hawaamini ya kwamba Yesu alikuwa ni Mungu. Nao walisema, kwamba, "Yeye alikuwa ni mtu mzuri, bali alikuwa ni mwalimu na mwanafalsafa, ila asingeweza kuwa Mungu."

36 Nikasema, "Kama hakuwa Mungu, Yeye alikuwa ni mdanganyifu mkubwa kuliko wote ulimwengu uliopata kuwa nao. Naam, bwana. Huwezi kufanya chochote kutoka kwake ila kwamba ni Mungu."

37 Akasema, "Kama nikikuthibitishia, kwa Biblia yako mwenyewe, Yeye hakuwa Mungu, je! utalikubali?"

Nikasema, "Huwezi kuthibitisha hilo kwa Biblia nisomayo."

Akasema, "Vema, nitakuonyesha."

Nikasema, "Vema."

38 Akasema, "Katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 11," kasema, "Biblia ilisema, wakati Yesu alipoenda kwenye kaburi la Lazaro, 'Alilia.'"

Nikasema, "Hakika."

Akasema, "Vema, angewezaje kulia, akiwa ni Mungu?"

39 Nikasema, "Vema, unashindwa tu kuona kwamba Yeye alikuwa ni nini. Wakati alipoenda kaburini, akiomboleza, Yeye alikuwa ni Mwanadamu. Lakini hapo alipoyavuta maskini mabega Yake pamoja, kasema, 'Lazaro, njoo huku,' naye mtu aliyekuwa amekufa siku nne, akatoka kaburini, huyo alikuwa ni zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mwanadamu." Mnaona? Kweli.

40 Alikuwa ni Mwanadamu wakati aliposhuka kutoka mlimani, ana njaa na akatafuta chakula mtini. Akaulaani huo mti kwa kuwa haukuwa na chakula. Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati alipokuwa na njaa. Bali alipochukua biskuti tano na samaki wawili, na kuwalisha elfu tano, wakaokota vikapu saba vilivyojaa, huyo alikuwa ni zaidi ya Mwanadamu. Huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mwanadamu.

Naye Mungu hujiwakilisha tu katika mwanadamu. Alimchagua mwanadamu.

41 Wakati alipokuwa amelala kwenye ule mtumbwi usiku ule. Ambapo, nguvu zilimtoka, siku nzima, akihubiri, huku watu wanamvuta, akifanya utambuzi, na kadhalika. Na tufani juu ya bahari. Nakisia pepo elfu kumi waliapa wangemzamisha, usiku huo, wakati alipokuwa amelala pale nyuma, amelala usingizi nyuma ya mtumbwi; hao wakirushwa-rushwa kama kifuniko cha chupa huko nje kwenye bahari yenye nguvu mahali fulani. Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati alipokuwa amechoka, amejilaza pale, akilala. Hiyo ni kweli. Lakini mara alipoamshwa, akauweka mguu wake demani mwa mtumbwi, akaangalia juu, kasema, "Amani, tulia," huyo alikuwa ni zaidi ya Mwanadamu pale. Naam. Huyo alikuwa ni Mungu katika Mwanadamu.

42 Alikuwa ni Mwanadamu wakati alipokufa msalabani, akilia apate rehema. Alikuwa ni Mwanadamu. Lakini wakati alipoivunja mihuri ya mauti, kuzimu na kaburi, kisha akafufuka siku ya tatu, Yeye alithibitisha alikuwa ni zaidi ya Mwanadamu. Ilikuwa ni Mungu ndani ya Mwanadamu. Si ajabu, kila mtu aliyepata kuwa chochote aliamini hilo. Washairi wote na kadhalika waliopata kuwa kitu chochote, waliamini hilo. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa ni zaidi ya Mwanadamu. Alikuwa ni Mungu.

43 Sasa, Mungu, ndani ya Mwanawe Mwenyewe, aliujenga mwili ambao Yeye aliishi ndani yake, amefanyiwa maskani, akabadilisha umbo lake. Wazieni tu. Yehova amelala horini, juu ya lundo la samadi katika banda, akilia kama mtoto mchanga. Maskini mikono hiyo ya kitoto, mtoto Yehova akishuka chini na kujificha katika—katika umbo hilo. Hebu mwangalieni Yehova huko nje akicheza, kama mvulana tineja. Mwangalieni Yehova akijenga katika duka la seremala. Yehova akining'inia msalabani. Kisha, alipofufuka, Yeye alithibitisha alikuwa ni Yehova. Hiyo ni kweli. "Mungu, katika Kristo,

aliupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Yeye alikuwa ni zaidi ya mwanafalsafa. Alikuwa ni zaidi ya nabii. Alikuwa Imanueli.

44 Sasa, usiku wa leo, tutaliendea hili, somo hapa. Vema, ndio kwanza tuyasome Maandiko. Nasi tutalichukua hili kama somo: *Basi Macho Yao Yalipofumbuliwa, Walimtambua*.

45 Sasa, onyesho letu linaanza kwenye wakati wa kupendeza, ama mandhari, ilikuwa yapata majira haya ya mwaka. Ilikuwa katika Pa—Pasaka. Nayo ilikuwa Pasaka ya kwanza, nzuri. Naye Yesu alikuwa amefufuka katika wafu, katika wakati wa majani kuchipuka, wa Pasaka, akiishi miongoni mwa watu tena. Nao wengi, waliompenda, hawakujua.

46 Na hivyo ni kama ilivyo leo hii. Wapo watu wengi wanaompenda, ambao kweli hawawezi kuamini kwamba Yuko pamoja nasi sasa. Wao, kamwe hawaonekani kulifahamu hilo.

47 Wao, naam, wengi wao kwenye siku hiyo, waliokuwa wametembea na kuzungumza Naye, wasingeweza kufahamu kwamba alikuwa amefufuka katika wafu, ingawa walikuwa na mashahidi, walikuwa wameenda kaburini, na kadhalika, na walijua alikuwa amefufuka katika wafu, bali hata hivyo wangali wasingeweza kuamini. Kwa nini? Nashangaa ni kwa nini. Mnaona, hilo si la kawaida kabisa. Mnaona? Kuna . . . Si la kawaida kabisa.

48 Na kwa kawaida Mungu huwa katika mambo yasiyo ya kawaida. Mambo yasiyo ya kawaida ndiyo yanayomfanya Yeye Mungu. Mnaona? Hayo ndiyo yanayomfanya kile alicho Yeye, ni mambo anayofanya yasiyo ya kawaida kabisa.

49 Sasa, lilikuwa ni jambo lisilo la kawaida wakati Yusufu, kabla ya kuzaliwa, wakati alipomwona Mariamu; maskini kipenzi chake cha kupendeza ambaye alikuwa amemposa, apate kumwoa. Alimwona, alikuwa ni mja mzito, pasipo kuolewa. Kwa hiyo yeye, hapana shaka, alikuwa amemwambia juu ya kuzuriwa na—na Gabrieli, Malaika. Naye Yusufu alikuwa ni mtu mwenye haki. Alikuwa mtu mzuri. Naye alikuwa—alikuwa hivyo. Alitaka kumwamini. Naweza kuwazia alimpenda kwa moyo wake wote, akimwona maskini mwanamwali huyo wa Kiebrania, na—na kuyaangalia macho yake, na—na aliposema, "Yusufu, mpenzi. Yule Malaika mkuu, Gabrieli, alinizuru, naye akasema nitatiwa 'uvuli na Roho Mtakatifu.' Nacho Kitu hicho Kitakatifu kitakachozaliwa ndani yangu, kitakachozaliwa kutoka kwangu, kitaitwa 'Mwana wa Mungu.'"

50 Sasa, yeye alitaka kuamini hilo. Bali hakukuwa kumewahi kuwapo na lolote lililotukia jinsi hiyo, kwa hiyo lilikuwa lisilo la kawaida mno. Pia, angalieni, huyo alikuwa ni mtu mwenye haki, mtu mzuri, huku Maandiko yakidai kwamba lingetukia, "bikira atachukua mimba," naye hakuelewa. Mnaona? Maandiko yaliyosema ya kwamba Kristo angezaliwa jinsi hiyo, bado,

Yususfu asingeweza kulielewa, kwa maana yalikuwa yasiyo ya kawaida mno.

51 Sasa katika siku hizo, wao hawakuwa na manabii. Mtu huyo alikuwa . . . Hawakuwa na manabii kwa mamia ya miaka, na kwa hiyo Mungu akamshughulikia katika ndoto. Ndoto ni njia ya pili. Njia ifaayo daima ni ya Neno, kwanza. Sasa, Mungu ana njia ya kuthibitisha kama Neno Lake ni kweli, ama si kweli. Ama mahali palipokuwapo na ninii yoyote . . .

52 Katika Agano la Kale, Aaroni alikuwa na mawe kumi na mawili, mawe ya kuzaliwa, kwenye kifuko chake cha kifuani hapa. Nao walikitundika kwenye nguzo hekaluni. Kama nabii alitabiri, ama mwotaji akaota ndoto, waliwapeleka kwenye hiki, kile kinachoitwa, kama vile wahudumu wangejua, Urimu Thumimu. Na kwa hiyo, hiki, mwotaji huyo aliposimulia ndoto yake, ama nabii akasimulia unabii wake, nazo nuru za kimbinguni hazikumulika juu ya hicho, kufanya Urimu Thumimu, basi, sijali ilisikika halisi jinsi gani, ilikuwa ni ya uongo. Ilibidi Urimu Thumimu ishuhudie kwamba ni kweli. Vema, huo, sasa, ukuhani wa Aaroni, uliondolewa, pamoja na Urimu Thumimu ya kale.

53 Lakini Mungu angali ana Urimu Thumimu, na hiyo ni Neno. Kama—kama nabii akitabiri, ama mwotaji aote ndoto, nayo ni kinyume na hilo Neno, sijali inasikika halisi jinsi gani, isahau. Hiyo ni Urimu Thumimu ya Mungu. Hiyo ndiyo. Nayo hiyo haina budi kujibu, ipate kuwa ni kweli. Hiyo ni kusema, Mungu alifasiri Neno Lake Mwenyewe.

54 Kwa hiyo, Mungu hakuwa na manabii nchini, siku hiyo, kwa hiyo Mungu akanena na Yusufu kwa njia ya pili. Ikionyesha, ya kwamba, endapo hakuna kitu kilichopo ambacho kingeileta, Mungu anaweza kutenda kazi kupitia kitu chochote, chochote ambacho ameahidi. Mnaona? Angeweza kutenda kazi kwa ndoto. Kama hapakuwapo na nabii, basi Yeye angeweza kutenda kazi kwa ndoto.

55 Kwa hiyo haidhuru karama zetu ndogo ni nini, Mungu anaweza kunena nasi kwa njia yoyote atakayo, bali haina budi kuambatana na Neno. Mnaona? Haina budi kuwa ni kulingana na Neno.

56 Sasa, tunaona ya kwamba ndoto yake ilikuwa ni kulingana na Neno, kwa kuwa Isaya alisema, "Bikira atachukua mimba," na ikawa. Ndoto yake ilikuwa ni kulingana na Neno, naye huyu ndiye aliyekuwa amepata mimba. Halafu wakati Ro—Roho wa Bwana, Malaika wa Bwana, alipomtokea, katika ndoto hii, na kusema, "Yusufu, ewe mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Mariamu mkeo, kwa sababu mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu." Vema, hilo lililitatua basi.

57 Yeye alikuwa ni mtu mwenye haki. Alitaka kuliamini. Alitaka kuliamini, bali lilikuwa lisilo la kawaida sana kwake.

58 Na kama mtu anataka kuamini chochote, na—na Kweli iko mbele zake, Mungu atafanya njia fulani ya kuthibitisha hilo, kuthibitisha kwamba ni Kweli. Mungu anawajibika kufanya hivyo, maana hiyo ndiyo sababu ya kumwokoa, ni wale waliokusudiwa Uzima.

59 Sasa, tunaona ya kwamba jambo hilo lisilo la kawaida lilikuwa—lilikuwa ndilo jambo ambalo—ambalo wasingeweza kupata. Nao ufufuo huu ulikuwa usio wa kawaida.

60 Hao, na, hata hivyo, kama wangaliangalia, lilikuwa ni Neno Lake lililoahidiwa. Alikuwa amewaambia, kasema, "Mwana wa Adamu anakwenda Yerusalemu, Naye atapata mateso mengi kwa Mataifa, na kutolewa mikononi mwao na kusulubishwa, kuzikwa; kisha atafufuka, siku ya tatu." Mnaona? Alisema, pia, "Kama vile Yona alivyokaa katika tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuwa katika moyo wa nchi, siku tatu mchana na usiku." Daudi, mmoja wa manabii wao, alitabiri, kasema, "Sitaiacha nafsi yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu." Mnaona? Na manabii wote walinena habari Zake.

61 Basi ilionekana kana kwamba wanafunzi hawa, bado, ilionekana kana kwamba wangeweza, wangeweza kulitambua, na iliwapasa kujua jambo hili. Lakini, mnaona, lilifichwa kutoka kwao. Nalo Neno lililoahidiwa kwao, hata hivyo hawakulitambua. Mnaona? Lilitimizwa, kile hasa Yeye alisema kingetukia, kile Agano la Kale lilichosema kingetukia. Kilitimizwa kikamilifu, na hata hivyo hawakuielewa.

62 Angalia, wakati wakiondoka sasa, wawili wao, Kleopa na rafiki yake walikuwa wameshika njia kwenda Emau. Na ilikuwa ni Jumapili asubuhi. Kwa hiyo walikuwa wakienda zao kule, wakizungumza. Walikuwa wameshika njia, wamehuzunika mno. Jamani, kweli walikuwa wameshushwa moyo na kitu fulani, kilionekana kama ni pazia.

63 Naye Mungu huachilia mambo yatukie namna hiyo. Yeye hufanya hivyo, makusudi, kuninii tu—kukujaribu tu. Sasa hebu niweke jambo hili mbele zenu, moja kwa moja, mpate kuelewa ya kwamba kila mwana amjiaye Mungu hana budi kufunzwa kama mtoto. Hana budi kujaribiwa; kila mwana. Iwapo hujapata kujaribiwa, wewe si mwana. Kama huwezi kustahimili marudio ya Mungu, basi wewe ni mtoto haramu, wala sio mtoto wa Mungu. Unadai Mungu Ndiye Baba yako, unasema, "Loo, siwezi kuamini." Vema, hiyo inaonyesha tu kwamba Mungu siye Baba yako; unaona, ungeninii—ungelipata. Sasa angalia, kujaribiwa huku, Mungu humjaribu kila mmoja wa watoto Wake. Wote wamjiao hawana budi kupimwa, kujaribiwa, kuthibitishwa.

64 Hebu mwangalieni wakati alipokuwa hapa duniani. Siku moja aliangalia kila mahali, umati mkubwa wa watu ulikuwa pamoja Naye. Loo, wakati alipoondoka kwa mara ya kwanza,

Yeye alipendwa sana. Makanisa yote yaliifungua milango yao. “Huyu Rabi kijana, mbona, hapana shaka ila Yeye ni Nabii mkuu aliyeinuliwa miongoni mwetu. Anawaponya wagonjwa wetu. Mbona, Yeye huja kwenye ibada hizi za uponyaji. Hutenda mambo makuu.” Hilo lilikuwa sawa. Lakini siku moja kulikuwako na wengi mno waliomfuata. Mnaona? Hiyo ilikuwa ni ishara ya kuvutia usikivu wa watu.

65 Sasa, Sauti haina budi kuifuata ishara hiyo. Hilo lilikuwa Fundisho Lake. Angalia. Lakini hapo Sauti ilipokuja, loo, hiyo ilikuwa ni tofauti. Jamani! Hao, walimsulibisha kwa sababu Yeye alijifanya sawa na Mungu. Alipokuwa akiwaponya wagonjwa, na kufanya miujiza, na kuyatambua mawazo moyoni mwao, hilo lilikuwa ni zuri sana. Bali hapo aliposema, “Mimi na Baba Yangu ni mmoja,” loo, jamani, Hilo lilikuwa limewazidia mno. Wasingeweza kulipokea Hilo. Mnaona? Walininii . . . Hilo lilizidi.

66 “Yeye hujifanya Mungu, kwa hiyo a—anajaribu kuwa sawa na Mungu.”

67 Vema, alikuwa. Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Naye alisema, “Mnawaita, ambao walijiliwa na Neno, torati yenu inasema kwamba, kwamba, ‘Neno liliwajia manabii,’ nanyi mnawaita ‘miungu.’ Basi, kama mngeweza kumwita nabii, ‘mungu,’ mwawezaje kunihukumu Mimi ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu? Yachunguzeni Maandiko; Hayo Ndiyo yanayowaambia kile ninachopaswa kufanya. Nisipofanya kulingana na yale Neno linayosema ninapaswa kufanya, basi msiniamini. Bali nikizifanya kazi za Baba Yangu, ambazo ni Neno, basi—basi aminini kazi nizifanyazo.” Hata hivyo wasingeamini.

68 Kwa hiyo, Yesu alisema, siku moja. Sasa angalieni. Yeye haelezei mambo. Anayasema tu. Angalieni. Alisema, “Msipoula mwili Wake Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu.”

69 Mngeweza kuwazia kile kundi zuri la watu wenye akili, kundi la madaktari waliosimama kule nje, na marabi, watu waliofunzwa na wenye elimu nyingi, walivyowazia, hapo aliposema hivyo? Loo, naweza kuwazia daktari aliangalia kule, kasema, “Whiu!” Wa—wahudumu wanaamka, wanasema, “En-he. En-he. Mnaona, Hilo, hilo lililiweka wazi, papo hapo.”

70 Sasa, Yeye hakuelezea Hilo. Kamwe hakulielezea. Haikumbidi kulielezea. Haikumbidi kulielezea.

71 “Mbona,” wakasema, “vema, mbona, anatufanya . . . Anataka tuwe wanadamu wafyonza damu, tunywe damu ya binadamu, na kuula mwili wa mwanadamu.”

72 Kamwe hakusema jinsi hilo lingefanyika. Alisema tu, “Msipofanya hilo!” Mnaona?

73 Halafu umati huo wa nje, maelfu, kasema, “A-ha. Huyo hapo. Mnaona? Naam. Nilijua lingejitokeza, baada ya kitambo kidogo.” Mnaona, walikuwa wakilitarajia litokee, Naye akahakikisha litatokea. Walikuwa ni kupe, kwanza kabisa, kwa hiyo hawakuambatana Naye tena.

74 Kwa hiyo, akageuka. Alikuwa pamoja na watu sabini. Kwa hiyo, akawaambia hao sabini, kasema, “Mtasemaje mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa Mbinguni mahali alipotoka?” Sasa, Yeye hakulielezea.

75 Waliangaliana, wakasema, “Vema, ati Mwana wa Adamu akipaa kutoka mahali alipotoka? Vema, tunamjua mama Yake. Tunawajua ndugu Zake, dada Zake. Tuliona hori alimolazwa alipozaliwa. Tuliona kitanda kidogo alimopembezewa. Mbona, Yeye ametoka Nazareti. Ati akitoka huko Juu? Hili ni Neno gumu.” Basi hawakutembea pamoja Naye tena. Mnaona?

76 Sasa, wakati wote, wanafunzi hawa walisimama pale pale. Wala nao hawakulijua, bali waliliamini. Wasingeweza kulielezea. Kamwe hakulielezea. Lakini, mnaona, walikuwa wamekusudiwa Uzima. Wasingeweza kulielezea, bali waliketi pale. Kwa hiyo aligeuka na kusema, “Nimewachagua kumi na wawili; mmoja ni ibilisi.” Akasema, “Je! mnataka kwenda, pia?”

77 Na hapo ndipo Petro alitamka maneno hayo yasiyosahaulika, “Bwana, tumeshawishika kwamba Wewe unalo Neno la Uzima, peke yako. Twende wapi?” Jambo lilikuwa hilo, mnaona. Mnaona?

78 Hakulielezea. Alisema hivyo kusudi walikatae. Mnaona? Imani haiulizi, haitoi hoja. Inayachunguza Maandiko kwa ajili yake. Kama wangaliyachunguza Maandiko, hapo ingalithibitishwa kwamba Yeye alikuwa ni nani. Bali Yeye aliwatikisia mbali namna hiyo, kwa kusema mambo pasipo na kuyaelezea.

79 Na uwanjani mle, hata, walipokiweka kitambaa hiki usoni Mwake, na wengine wakampiga na kumchapa. Kasema, “Kama—kama Wewe ni nabii, twambie ni nani aliyekupiga sasa, na—nasi tuta—tutakuamini.” Jambo lile lile, ibilisi yule yule wa kale a—aliyekuwa huko juu, wakati wote, wakati alipojaribiwa, wakati alipoanza huduma Yake kwa mara ya kwanza. Kasema, “Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, yaamuru mawe haya yawe mkate.” Yeye yule. Nao hao makuhani na marabi kule juu, kasema, “Kama Wewe Ndiye Kristo, shuka utoke Msalabani na kututhibitishia sisi.” Mnaona? Angaliweza kufanya hivyo. Alijua ni nani aliyempiga, bali hamfanyii mtu yeyote vitimbi.

80 Yeye alikuwa ni Neno, na angali ni Neno. Daima alikuwa ni Neno, na anabaki ni Neno. Wangalirejea huko nyuma, wangaliweza kuona Hilo, bali hawakurejea.

81 Walikuwa, angalieni, wameshika njia. Walikuwa nini? (Wale wanaoketi hapa, ninawatakeni msikilize kwa makini.) Walikuwa wakizungumza habari Zake wakati alipowatokea.

82 Sasa, hivyo ndivyo Yeye huja, ni wakati unapozungumza juu Yake. Shida, leo hii, tunazungumza juu ya mambo mengine mengi mbali Naye. Daima tunazungumza juu ya yale tunayopaswa kufanya, na shughuli fulani ya biashara, ama nguo zinazopaswa kufuliwa, ama aina hii ya sabuni unayopaswa kutumia. Wakati, mnapaswa kuwa mkimpa sifa na utukufu. "Hapo ndipo palipo na hazina zetu, hapo ndipo roho yetu ilipo pia."

83 Walipaswa kumtambua, bali hawakumtambua. Na ndivyo ilivyo leo hii. Hata hivyo, Maandiko yalisema. Mnaona?

84 Yeye—Yeye aliwafunulia ahadi za Maandiko zilizomhusu Yeye kwa ajili ya wakati huo. Kumbukeni, Yeye alianzia na hapo mwanzo. Akasema, "Enyi msiofahamu na wenye mioyo mizito." Akawaelezea Maandiko. Na baada ya Maandiko kuhubiriwa kwao, hata hivyo hawakumtambua. Kama hilo si kusanyiko la—la kisasa, sijui. Wao, Maandiko, walielezewa, na hata hivyo wangali hawakuyapata. Walikuwa wakitembea moja kwa moja, walidai kuwa ni wanafunzi Wake. Hata hivyo, hawakumtambua kamwe, baada ya kuwaambia Maandiko ya wakati huo, ambapo Mungu alikuwa ameugawa.

85 Akasema, "Hivi hamjui kwamba Kristo alipaswa kupata mateso haya, na kuingia katika utukufu Wake na kufufuka tena? Yeye. . ." Iliwapasa kuona. Kasema, "Hivi hamjui yote manabii waliyosema juu ya Kristo?" Naye akaanzia huko nyuma, na kuwaelezea jambo hilo lote, na kuliweka mbele zao. Na hata hivyo hawakulitambua, baada ya kuyaelezea Maandiko kikamilifu tu iwezavyo kuwa. Nao wakiliepa, waliodhaniwa kwamba ni wanafunzi Wake, "Loo, loo, ndivyo ilivyo? Ndivyo ilivyo?" Na, hata hivyo, Yeye alikuwa Ndiye Andiko hilo lililotimizwa, amesimama pale, na hata hivyo hawakulipata. Mnaona?

86 Sasa hiyo ni picha nzuri sana ya siku tunayoishi. Sisemi hilo kwa ubaya. Ninasema hilo kwa ajili ya Kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

87 Wangali hawakumtambua, ingawa ahadi Zake alizokuwa amefanya zilitimia. Naye alikuwa akiwatangazia, huku amesimama pale Mwenyewe, na hata hivyo hawakumtambua.

88 Angalieni shutuma kwao kwa ajili ya kutoyatambua Maandiko yaliyotimizwa.

89 Sasa, wakati, walipaswa kujua. Walikuwa ni wanafunzi. Walikuwa ni watu waliojitolea sana. Walikuwa ni watu waliompenda. Walikuwa ni watu waliofunzwa Naye. Na, hata hivyo, baada ya Yeye kuwaambia mambo haya, kusimama kwenye kundi lao na kusema jambo hili lingetukia, nalo hili hapa

limetukia, na, hata hivyo, hao wakiwa wamesimama pale pale pamoja Naye baada ya kufufuka Kwake, wala hawakumtambua.

90 Mnasema, "Hivi tungeweza kufanya jambo kama hilo?" Ingewezekana tungefanya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Hakika ingewezekana. Baada ya Yeye kuahidi katika Neno Lake, jambo ambalo atafanya, nasi tunaliona likitimia jinsi tu Yeye alivyosema, na hata hivyo tunalipuuza. Hivyo ndivyo walivyokuwa wamefanya.

91 Sasa, Yeye alikuja moja kwa moja, akawaambia Yeye atasulibishwa, afufuke siku ya tatu, kisha akaanza kuwaambia yote kulihusu.

92 Nao walikuwa na huzuni, kasema, "Unajua, baadhi ya jamaa hao walishuka wakaenda kaburini, na baadhi ya wanawake. Walisema angefufuka katika wafu. Na uvumi huu wote umeenea kote." Ndipo kasema, "Wewe ni mgeni tu huku? Hujui mambo haya?"

93 Akasema, "Mambo gani?" kana kwamba tu hakujua lolote kulihusu. Mnaona, Yeye alisema hivyo, kuwatupilia mbali tu. Naye akafanya hivyo, makusudi, kujaribu tu.

94 Basi hivi hamjui Yeye habadilishi tabia Yake? Yeye hufanya jambo lile lile, kuninii tu—kukujaribu tu, aone vile utakavyofanya. Yeye atafanya kazi kwa njia fulani, itatupwa mbele zako, apate tu kuona yale—yale utakayosema kulihusu, msimamo wako, jinsi unavyolichukulia, yale unayoliwazia. Yeye hufanya hivyo, makusudi, angali analifanya, kwa sababu hiyo ni tabia Yake isiyobadilika. Alifanya hivyo zamani za kale.

95 Kumbukeni Eliya. Hata alimfanya askari ampige kofi. Akasema, "Nilikuwa mlinzi, nikisimama karibu, na Ahabu, nami nikamwachilia mfungwa atoroke." Hakufanya hivyo, bali alifanya hivyo kusudi amwache Ahabu atoe hukumu yake mwenyewe.

96 Alifanya jambo lile lile katika siku za Nuhu, na Yeye—Yeye hawezi kubadilisha njia Yake. Naye Mungu hushuka kwa njia fulani. Lakini daima . . .

97 Mnasema, "Vema, ningewezaje kujua ukweli na uongo?" Ni Maandiko yaliyoahidiwa kwa ajili ya wakati huo. Ni Maandiko yaliyoahidiwa.

98 Laiti wangalitoka kwenye mapokeo yao, na kuyaacha mapokeo hayo waliyokuwa nayo, na kuyasoma Maandiko, kama alivyowaambia wafanye! "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yao mnadhani mna Uzima wa Milele, Nayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yanawaambia kwamba Mimi ni Nani."

99 Nao wakasema, "Vema, sasa, rabi alitwambia *hili* na *lile*. Sisi, sisi tunaamini yale kanisa lisemayo." Mnaona?

100 Si yale kanisa lisemayo. Ni yale Mungu aliyosema. Yale aliyosema Mungu, si yale dhehebu lisemayo, ama hayo. Wewe

mwamini Mungu. Sasa, hapo ndipo waliposhindwa, kwa kuwa walikuwa wameshika mapokeo sana hata wakashindwa kulitambua.

101 Sasa tunaona, basi, Yeye alisema aliwakemea. Angalieni. "Enyi msiofahamu na wenye mioyo mizito kufahamu ishara zote za Kimaandiko na kadhalika zinazopaswa kutukia kwenye wakati huu. Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito kufahamu yote ambayo manabii wamesema kwamba yanapaswa kutukia katika siku hii, ishara hizi zote mnazoona. Biblia ilisema ishara hizi zilipaswa kutukia kwenye siku hii, nanyi mnaziona zikitimia, halafu ninyi ni wasiofahamu vya kutosha msiziamini?" Naye akizungumza nao ana kwa ana, na hata hivyo hawakulitambua. Nena kuhusu upofu!

102 Tungeweza kufanya hivyo? Huenda tungeweza, kama hatuyachunguzi Maandiko, kutafuta kujua saa tunayoishi, kuona ni saa gani, ni nini, jinsi gani. Huenda imechelewa kuliko tunavyowazia imechelewa.

103 Hata hivyo, walidai kwamba ni wanafunzi Wake. Walidai kuamini ya kwamba walikuwa wameliamini kila Neno ambalo alikuwa—alikuwa amesema. Waliiamini Biblia nzima. Naye huyu hapa—huyu hapa Masihi, Mungu wa Biblia, amesimama pale katika utambulisho, akilitambulisha Neno lenyewe lililoandikwa. Nao walidhaniwa kuwa ni waaminio wa Neno hilo. Naye akirejea nyuma, na kuwaambia hilo. "Mnakumbuka yale yaliyosemwa kuhusu hili; na yaliyosemwa kuhusu hili; na jinsi ambavyo Yesu hana budi kufanya hivi; ama jinsi Kri— Kristo hana budi kufanya hili; na jinsi ambavyo basi mambo haya yote?" Na hata hivyo hawakulielewa. Hawakujua. Ilikuwa ni kitu gani? Walilijua Neno, tukinena habari za waraka, bali hawakulifahamu Neno wakati lilipofasiriwa dhahiri.

104 Hivyo ndivyo ilivyo leo hii. Kila mtu ana fasiri yake mwenyewe. Wakati, Mungu anahukumu kitu hicho chote. Mungu hujifasiria Mwenyewe. Kama Mungu alisema atafanya jambo fulani; wakati anapolifanya, hiyo ndiyo tafsiri yake. Mungu hulifasiri Neno Lake Mwenyewe.

Huyo hapo, amesimama pale, Yeye Anayejifasiria.

105 Haleluya! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye hujifasiria Mwenyewe. Hahitaji seminari yoyote, wala wahudumu wowote, mimi, wewe, wala mwingine yeyote, kumfasiri. Yeye aliliahidi, ndipo anageuka na kulifanya. Hilo latosha. Hilo linajifasiri lenyewe.

106 Lakini huyo hapo amesimama, yule mwenye nguvu mkuu, Mshindi wa kila ugonjwa, kila maradhi, mauti, kuzimu, kaburi. Naye alifufuka tena, kile walichokuwa wameamini wakati wote. Naye huyo hapo amesimama, wala wasingeweza kuamini. Naye huku anarejea kwa Nafsi Yake Mwenyewe wakati wote, akawaambia. "Akaanza kutoka Musa na manabii,

akawafafanulia mambo yote yaliyoandikwa kumhusu Yeye Mwenyewe," na bado hawakulipata. Ilionekana tu kana kwamba wasingalilipata kamwe. Hivyo tu.

107 Vivyo hivyo sasa. Kuna shida gani, leo, sababu yake? Tunashughulika sana na kujifunza kanuni zetu za imani. Tunajishughulisha sana na mipango ye—yetu ya kimadhehebu. Tunashughulika sana na karamu za supu na bahati nasibu kanisani. Tunashughulika sana na shirika la wanawake la msaada. Tunashughulika sana na vipindi vyetu vya TV na upuuzi huu mwingine wote. Tuna shughuli nyingi sana tusingeweza kuyachunguza Maandiko, tujue kama ni ya kweli ama si ya kweli.

108 Ungalishuka uende kwenye mkahawa na kuagiza bakuli ya supu, nayo ilikuwa na buibui ndani, ungeushtaki mkahawa huo. Usingeinywa kwa vyovyote, ikiwa na buibui, maana unahofu huenda ikauua maskini mwili huu.

109 Lakini utasukumiza chochote ndani ya nafsi hiyo, chochote tu, kanuni ya imani ya namna yoyote, wala hukuichunguza kamwe, uone kama ni ya kweli ama sivyo. "Iko njia ionekanayo sawa machoni pa mtu." Yachunguzeni Maandiko. Nafsi hiyo ni ya Milele, mwajua. Kwa hiyo, usithubutu. Angalia tu kile unachoingiza mle, unaona, kanuni hizi za imani na vitu hivi vyote. Tumelifanya tu kama chama, kujiunga tu na chama na hiyo yatosha. Na hivyo ndivyo watu wanavyowazia siku hizi. Hiyo ndiyo sababu hawana wakati wa kusoma, kutafakari, kuchunguza mambo, na kujaribu kuona kama ni ya kweli au la.

110 Acha Kristo Mwenyewe alifasiri. Na kama likitimia, kile alichosema, basi hiyo ni Kweli. Angalia uone kama ni la siku hii.

111 Kama nilivyorejea jana usiku, Musa asingeweza kuja na ujumbe wa Nuhu. Wala Yesu asingeweza kuja na—na ujumbe wa Musa. Mnaona? Ulikuwa hivyo, ulikuwa umetengwa kwa ajili ya kila wakati.

112 Sasa, tusingeweza kuja na ujumbe wa Luther, wala wa Wesley, wala na ujumbe wa Kipentekoste. Tumeupita huo kabisa.

113 Mnasema, "Loo, hicho ni kitu ambacho unaninii . . . " Vema, vivyo hivyo na kanisa Katoliki liliwazia Luther alikuwa akiubuni. Vivyo hivyo Wesley alifikiri wananii . . . Walutheri walifikiri Wesley alikuwa akiubuni. Vivyo hivyo wa Wesley walifikiri Pentekoste ilikuwa ikiubuni.

114 Lakini jambo ni kwamba, rejeeni kwenye Maandiko. Yanatambulisha, kila wakati. Na kama mambo anayofanya sasa hayamtambulishi, zile ahadi za Mungu, basi achaneni nazo. Lakini kama akisema litatukia, nalo linatukia, basi amini kwamba si mwanadamu. Ni Mungu akinena, akitoa fasiri Yake Mwenyewe ya Neno Lake.

115 "Enyi msiofahamu na wenye mioyo mizito kuamini yote ambayo manabii wamesema kumhusu Kristo." Hata hivyo, wanafunzi Wake wasingeamini Neno lililoandikwa, kwa kuwa walikuwa na shughuli nyingi sana kuhusu, loo, vema, liliwahuzunisha.

116 Hata hivyo, wanadai wanaamini, leo, ya kwamba Yeye alifufuka siku ya tatu. Tunanena habari zake, "Loo, tunaamini ya kwamba Yeye alifufuka, siku ya tatu, Naye yu hai milele." Hebu afanye jambo fulani kama tu alivyoahidi atafanya, angalieni yale wanayosema, "Vema, ama ni kundi la watakatifu wanaojifingirisha, au ni kuwasiliana kimawazo, ama ni namna fulani ya mpiga ramli. Ama . . . " Kama tu walivyofanya wakati huo. Mnaona, ni roho yule yule. Sasa, kumbukeni, ibilisi humchukua mtu wake bali sio roho yake, roho iliyokuwa juu ya hao watu kule nyuma, walimu wa kidini.

117 Kumbukeni, hakuna mtu angaliweza kuwaelekezea kidole hao Mafarisayo. Ilibidi waishi maisha mema. Wangepigwa mawe wafe kama hawakuyaishi. Walikuwa ni wazuri, watu wazuri, walimu wenye elimu nyingi, wasomi. Naye Yesu akasema, "Ninyi ni kundi la nyoka. Mnatenda kazi za baba yenu." Mbona, mbona Mtu, Mungu, kamwe kumfasiria mtu wa namna hiyo? Angewezaje kusema jambo kama hilo? Kwa kuwa walikataa kuona Neno lililotambulishwa likidhihirishwa.

118 Sasa, leo hii, tumekuja, mara nyingi tumesema, Wa— Walutheri walisema, "Unapomwamini Bwana Yesu Kristo, umempata. Hivyo tu." Wanazarayo, na Wapilgrim Holiness, na Wamethodisti Huru, walisema, "La, huna budi kupaza sauti, kumpata." Wapentekoste wanasema, "Huna budi kunena kwa lugha, kumpata." Yote hayo si kweli.

119 Nimewaona wachawi wakinena kwa lugha, na walozi. Nimewaona wakiruka na kupaza sauti, na kuwaona Waislamu wakitoboa vidole vyao kwa vibanzi, na kupiga mayowe kuliko nilivyopata kuwasikia Wapentekoste maishani mwangu.

120 Lakini, hata hivyo, kuamini ni sawa, kunena kwa lugha ni sawa, na kupaza sauti ni sawa, na kushangilia. Ila hilo silo, bado.

121 Hao Mafarisayo, baadhi yao walisema, "Vema, ni tunda la Roho, hiyo ni kweli." Hao Mafarisayo walikuwa na matunda mengi zaidi ya Roho, yale tunayoita tunda la Roho, kuliko wangaliweza, tungaliweza kuzaa.

122 Ni nani atakayesema, kama nilikuwa nimweke mahakamani sasa, tuseme kama maskini jamaa fulani alivyoingia humu mjini hivi majuzi na kujiita nabii? Hebu tumweke mahakamani kwa dakika moja. Na sasa ninazungumza nanyi enyi watu, dhidi Yake; Mungu anisamehe kwa kusema jambo kama hilo, lakini kusudi tu nieleze jambo muhimu. Nasema, "Jamaa huyu mdogo, Yeye yuko mahali fulani hapa. Anajiita nabii. Anatoka Galilaya. Anafanya uponyaji mwingi sana na kadhalika, bali hilo halina

maana yoyote. Angalieni hapa juu, tuna birika la Bethsaida. Walemavu hukaa pale, wakati yule Malaika anaposhuka na kuyatibua maji, mtu yeyote huingia ndani. Kwa nini Mungu apende kitu kingine mbali na hicho?" Mnaona, wanashindwa kutambua Neno la siku hizo. Ahadi ilikuwa tayari kutimizwa.

123 Sasa wanasema, "Tutamhukumu kwa tunda la Roho. Sasa, angalieni, ni nani aliyesimama hapo karibu? Ilikuwa ni nani, wakati ulipokuwa huko nje ukitangatanga, kama kijana mwanamume, aliweka wakati wake wote kulisoma Neno la Yehova? Maskini kasisi wako mtauwa. Ilikuwa ni nani, wakati baba na mama walikuwa karibu kutengana, wakakumbatiana, mmoja akamkumbatia mwingine, na kuwapatanisha? Maskini kasisi wako mtauwa. Kweli. Ilikuwa ni nani, wakati mazao ya baba yako yalipoharibika, naye hakuwa na fedha hata kidogo, hamkuwa na chakula; ni nani aliyemwandikia hundi na kumpa fedha, ama wa kumsaidia? Maskini huyo kasisi mtauwa. Ni nani aliyesimama karibu na mama na baba yako, ulipozaliwa, wakati ulipokuja humu ulimwenguni kwa mara ya kwanza? Maskini huyo kasisi mtauwa. Ni nani aliyekushika mikononi mwake na kukutahiri, kwenye siku ya nane, na kuyakabidhi, maisha yako, kwa Mungu? Maskini kasisi mtauwa.

124 "Halafu, angalieni, kuna wafanya biashara hapa mjini kwetu. Yehova anahitaji mwana-kondoo. Hawa wafanya biashara ni watu wa bidhaa. Wanauza, uchuuzi, kwa hiyo haiwabidi—haiwabidi, kufuga wana-kondoo. Kwa hiyo kuhani alifanya njia ambapo wangeweza kuziosha nafsi zao, kulingana na Neno la Mungu, nao wakajenga vizimba vidogo huko nje uani. Nao wakamleta mtu aliyeuza wana—wana-kondoo, humu ndani, kisha akawaruhusu watu hawa wanaotaka kutoa dhabihu ya dhambi kwa ajili ya nafsi zao, masharti ya Yehova, wakati wanapokwenda kununua mwana-kondoo huyu.

125 "Basi Jamaa huyu alifanya nini alipopanda kule? Alizivuruga meza za pesa, na kuwapiga akawafukuza kule, akijaribu kuwazuia watu kuziweka nafsi zao sawa na Mungu. Naye alisema nini juu ya maskini huyo kasisi wenu mtauwa? 'Walikuwa ni kundi la nyoka, na ni wa ibilisi.'" Ati kunena kuhusu tunda la Roho? Wangelimshinda, kwa mbali sana.

126 Lakini ushahidi wa mwaminio ni nini? Kwamba hatafanya kitu ila kuamini Neno lililotambulishwa la wakati huo. Imekuwa hivyo daima. Watu hulivuruga, katika kila namna ya mapokeo, na dini, na madhehebu, na elimu, na kadhalika. Lakini Mungu anakuja, na Neno Lake, na kulithibitisha kwa ajili ya wakati huo. Huo ndio ushuhuda.

127 Mwangalieni muone. Yeye alisema, "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, msiniamini Mimi. Yachunguzeni Maandiko, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele; Hayo ndiyo yanayoshuhudia kwamba Mimi ni Nani. Nisipofanya yale

Maandiko yanayosema nitafanya, basi msiniamini Mimi." Mnaona? Na hata hivyo hawakujua. Na baada ya kutembea pamoja Naye, na hapa anajitambulisha Mwenyewe baada ya ufufuo, na kuonyesha ya kwamba, kwamba alikuwa Ndiye, kwa Maandiko.

128 Hata hivyo, mwajua, leo, baada ya jambo hilo, Yesu amefufuka katika wafu na kuwatokea watu katika siku za mwisho.

129 Wakati, hao walisema, miaka kadhaa iliyopita, wakati kundi la Pentekoste lilipoanza kwa mara ya kwanza, "Hakukuwako na kitu kama hicho." Ndilo kanisa linalopanuka upesi kuliko yote ulimwenguni, la Kipentekoste. Ni ujumbe ambao wamekuwa nao sasa kwa muda wa miaka hamsini. Wao walisema, "Isingewezekana," bali ilitendeka, haidhuru. Walisema, "Hakukuwako na kitu kama Roho Mtakatifu." Watu wakapiga hatua, wakampokea, vivyo hivyo tu. Mungu aliahidi ya kwamba angeimwaga Roho Yake. Utaikomeshaje, wakati aliahidi angeimwaga? Walisema, "Hakuna mtu atakayeliamini," bali waliliamini.

130 "Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu wototo, ambao wataliamini Neno Lake."

131 Walisonga mbele moja kwa moja. Wakawa kanisa lenye nguvu kuliko yote yaliyopo nchini. Mgeni Wetu wa Jumapili, lile Mgeni la Katoliki, lililotolewa, lilisema sio muda mrefu uliopita, kwamba, "Kanisa la Kipentekoste ndilo kanisa linalopanuka haraka kuliko madhehebu yote." Kasema, "Kanisa lao lilishuhudia wongofu wa watu milioni moja katika mwaka uliopita, nalo la Kipentekoste lilikuwa na milioni moja na mia tano elfu mwaka jana." Hiyo haijumlishi wangu, wa Roberts, na hiyo mikutano mingine kama hiyo. Mnaona? Ni wale tu ambao wanaingizwa kama—kama wafuasi. Baadhi yao, hao hawajui mahali wanapoishia, katika mikutano hii ya kiinjilisti. Lakini walisajili waongofu milioni moja na mia tano elfu katika mwaka mmoja, ilivyoshuhudiwa na kanisa Katoliki. Mnaona?

132 Walisema isingewezekana, na sasa Wapresbiteri, Wamethodisti, na Wabaptisti, wanamtafuta. Nao Wapentekoste ni vipofu vya kutosha kutoyaona majira haya. Hivi hamjui? Kwenye hiyo zamu ya saba, hapo wanawali waliolala waliposema, "Njoni, tupeni Mafuta yenu kidogo." Na wakati yeye, wao walisema, "Tunayo ya kututosha sisi wenyewe tu." Basi walipokuwa wakijaribu kuyanunua, Bwana arusi akaja, nao wakaingia. Haya basi. Mnaona?

133 "Na enyi msiofahamu," hivi angeweza kusema tena, "wenye moyo mzito kuamini yote Maandiko yanayosema kuhusu siku hii; kuamini ya kwamba wakati huu wa kanisa la Laodikia, kwamba Yeye amewekwa nje ya kanisa, na kwa sababu, 'Sisi ni tajiri, hatuna haja ya kitu'"?

134 “Vema, sisi ni moja ya madhehebu tajiri kuliko yote ulimwenguni, huduma ya Kipentekoste. Loo, jamani! Tulikuwa huko chini kichochoroni, lakini, ndugu, liko kwenye barabara ya mbele sasa, makanisa mazuri kuliko yote, na seminari zilizo nzuri kuliko zote. Nasi tunajenga moja, la dola milioni hamsini, papa hapa sasa, mnaona, na kila namna ya mambo makuu. Tajiri!”

135 Lakini hapo ndipo mnapoisahau ile ahadi. Mnaanza kuelekea kwenye mapokeo. Na hiyo ndiyo sababu, wakati Yeye anapokuja kujitambulisha Mwenyewe, watu wametiwa ganzi kabisa, kwa elimu yao na falsafa na kadhalika. Wamegeuza A—Amri za Mungu zikawa ni mapokeo. Ukisimama na kusema nao, na kabisa halikolei hata kidogo; linarudi. Sasa, kama likija limepigwa msasa sana, kama askofu fulani mkuu ama mtu fulani akileta kitu kama hicho, vema, wa—wangekipokea. Lakini, mnaona, kamwe halikuja namna hiyo. Kama madhehebu fulani yangeliendea, ingekuwa ni sawa, bali kamwe Yeye hakufanya hivyo. Hakulifanya.

136 Kama alikuwa amekuja pamoja na Kayafa, naye Kayafa angalikuwa amesema, “Sasa, mimi ni Masihi. Mimi ndimi ninayepaswa kuja sasa.” Mnaona, wangesema, “Loo, baba mtakatifu mkuu, wewe ndiye Masihi.” Lakini, mnaona, hiyo haimtambulishi Masihi. Haki za—zake za dini, hizo hazikumfanya Masihi.

Alikuwa ile ishara Biblia ilisema ingemfanya Yeye Masihi.

137 Hivyo ndivyo ilivyo tena leo hii. Sio madhehebu yetu, wala kanuni zetu za imani, bali kwamba BWANA ASEMA HIVI ni nini. Sasa angalieni.

138 Vivyo hivyo sasa, tunajikuta wenyewe jinsi ile ile, tungali tunaamini kanuni za imani, dhehebu, na elimu ya kilimwengu, kadhalika. Mbona, mwajua, mengi ya makanisa yetu yameanza kukubali wazo kwamba kabla mmishenari hajaweza kwenda hudumani, basi inawabidi kufanyiwa uchunguzi wa akili na daktari wa akili, waone kama IQ yao ni ya juu kutosha kuwa wamishenari. Sasa, hiyo ni kinyume na Maandiko.

139 Biblia ilisema ya kwamba Petro alikuwa ni mtu asiye na elimu wala maarifa. Hata asingeweza kuandika jina lake mwenyewe. Bali ilimpendeza Mungu kumpa funguo za Ufalme, kwa kuwa alimwona Masihi na akajua ushuhuda wake, na kuanguka miguuni Pake na kumtambua Yeye kama Masihi. Yeye aliliamini Neno. “Nawe ndiwe Petro. Nakwambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.” Sio juu ya Petro, sio juu ya Yesu, bali juu ya ufunuo wake wa kiungu ya kwamba Yeye alikuwa ni Nani.

140 Jambo lile lile alilofanya Habili. “Habili kwa imani alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora sana kuliko ya Kaini.” Wavulana wote wawili walitoa. Wavulana wote wawili waliomba. Wavulana

wote wawili walijenga madhababu. Wavulana wote wawili walimwabudu Mungu yeye yule. Mnaona? Mmoja alikubalika, huyo mwingine akakataliwa. Kwa sababu, kwa ufunuo, Habili aliona haikuwa ni matunda wala matofaa yaliyotutoa kwenye bustani ya Edeni. Ilikuwa ni damu. Naye akatoa damu, na Mungu akaipokea.

141 Basi angalia—angalia huko Moabu, lile dhehebu kuu. Mungu yeye yule! Huyu hapa Balaamu anakuja, askofu, anatoka, akajenga madhahabu saba kama yale tu Israeli waliyokuwa nayo kule chini. Akaweka dhabihu saba safi, ng'ombe dume, na kondoo waume saba, wakinena juu ya Kuja kwa Kristo. Kimsingi, wote wawili walikuwa sahihi. Lakini angalia hapa chini kwenye maskini kundi hili dogo la wahaini linaloelea huku, hata wasingepitia nchini. Mchungaji wake anahofu watakuwa na namna fulani ya uamsho kule juu, kwa hiyo wasingewaruhusu kupita. Wakienda zao kwenye nchi ya ahadi, pia, wala asingemruhusu ndugu yake, Israeli, kupita. Kweli. Yeye . . .

142 Kile Balaamu alichoshindwa kuona ni ule Mwamba uliopigwa na yule nyoka wa shaba, kelele za Mfalme kambini. Wanashindwa kuona ule utambulisho wa Mungu miongoni mwao. Wote wawili walikuwa na manabii; Balaamu huko juu, na Musa hapa chini. Lakini Musa alitambulishwa na Neno. Hiyo ndiyo tofauti. Wote wawili ni wahubiri mashuhuri, bali mtu huyu alitambulishwa na Neno. Yeye hakuwa taifa kuu, kama huyo alivyokuwa. Bali alitambulishwa na Neno, na alikuwa na thibitisho Lake. Amina.

143 Hilo ndilo kundi halisi linaloamini: Kristo pamoja nasi; Kristo ndani yetu. "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; bali nyinyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Angalieni.

144 Sasa kumbukeni, upesi. Walishindwa kuliona. La, hawakufahamu, jinsi ingeweza kuwa. Nalo Neno lililoahidiwa lilikuwa ni kwa ajili ya wakati wao. Yeye alikuwa ni ile ahadi iliyotimizwa, na hata hivyo wakashindwa kuiona, ishara halisi ya nabii wa kweli. Angalieni alichofanya. Nao . . . Sasa angalieni. Walienda upesi . . .

145 Akasema, "Wewe, ukiwa mgeni, wala hujui ya kwamba Yesu wa Nazareti, Nabii wa kweli, mwenye nguvu mbele za Mungu pamoja na watu? Tunaamini na tunajua Yeye alikuwa ni Nabii." Mwangalieni, mara walipomtambua.

146 Aliendelea kuuliza, "Ati nini, mambo haya yaliyotukia? Nini, ni nini iliyotukia."

147 Akasema, "Yesu wa Nazareti, mtu Nabii, mwenye uwezo mbele za Mungu na za watu. Nasi tulitumaini ni Yeye Ndiye atakayeiletea Israeli ukombozi."

148 Na mara walipomtambua kama Nabii, angalieni, mara aliingia kwenye Neno. I—ishara halisi ya nabii wa kweli. Nabii halisi huenda kwenye Neno, daima, kwa maana Neno la Bwana humjia nabii. Mnaona? Naye anaenda kwa. . .Basi angalieni alichofanya. Walimwambia kwamba waliamini kwamba Yeye ni Nabii. Sasa, inampasa, inambidi nabii, kujitambulisha Mwenyewe kwa Neno, amina, maana Neno daima humjia nabii.

149 Mzee Dk. Davis aliyeketi hapa, angalia; ambaye, sijui kama yupo ama hayupo. Nafikiri yuko huku chini Florida, mahali fulani, waliniambia. Dk. Davis, kama upo hapa, yeye ndiye aliyeniweka wakfu kwenye kanisa la Baptisti ya Kimishenari. Tulizoea kubishania Maandiko. Basi alisema, kwamba, "Yohana Mbaptisti alimbatiza Yesu, kwanza. . .Ama, Yesu alimbatiza Yohana, kwanza, kwa maana Yohana kamwe hakuwa amebatizwa. Naye alikuwa akihubiri ubatizo, wala hakuna mtu mwingine aliyestahili kumbatiza, kwa hiyo Yesu akambatiza Yohana," kasema, vema, "Alimruhusu." Vema, nisingeweza kuingiza hilo moja kwa moja niani mwangu, jinsi alivyofanya hilo. Nisingeweza kuyapata Maandiko.

150 Siku moja tulipokuwa peke yetu, Naye Malaika wa Bwana alikuwapo, Yeye alinifunulia.

151 Mnaona, sasa, angalieni. Yesu alikuwa ni Neno; Yohana alikuwa ni nabii. Hao hapo wawili walio wakuu sana duniani; Mungu na nabii Wake. Naye Neno alikuwa ni Mungu na daima inapasa, kwa Neno, kumjia nabii. Naye Yohana alikuwa ni nabii. Basi huyu hapa Neno anakuja moja kwa moja kuingia majini, kwa nabii. Neno linamjia nabii, majini. Amina. Najisikia kubarikiwa. Neno kabisa humjia nabii. Naye Huyu hapa, Neno katika umbo lililo hai; naye huyu hapa nabii; amesimama ndani ya maji. Nalo Neno likamjia nabii. Ninaweza kuyaona macho yao wakati wakikutana.

152 Yohana akaangalia juu, akaona mbingu zikifunguka, yule hua akishuka kama mabawa ya moto yakija juu Yake. Sauti ikitoka Kwake, ikisema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu ambaye ninapendezwa kuishi ndani Yake."

153 Wakati Yohana alipoangalia, aliiona ile Nuru juu Yake, vyovyote ilivyokuwa. Kwanza, wakati alipotembea ufukoni, yeye alisema, "Tazameni Mwana-kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu."

154 Yeye alihusika kikamilifu sana, imani halisi, akasema, "Kuna Mtu anayesimama miongoni mwenu, ambaye sistahili kuvibeba viatu Vyake. Yeye atabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto." Yeye alijua Huyo hana budi kuja katika siku zake, kwa kuwa Yeye alikuwa Mtangulizi Wake. Akasema, "Kuna Mtu miongoni mwenu sasa, msiyemjua. Bali mimi nitamjua, moja ya siku hizi, nitakapoiona ile ishara ikimtambulisha."

Ndipo Yesu akajitokeza, siku moja.

155 Akasema, “Yule pale Mwana-kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu.”

156 Yesu akaenda, yule Neno, moja kwa moja kwa nabii, majini. Yohana akamwangalia, katika unyenyekevu. Akasema, “Nina haja ya kubatizwa na Wewe. Mbona Wewe waja kwangu?”

157 Angalieni hili sasa, Neno na nabii, pamoja. Mnaona, itambidi nabii kulijua Neno, kwa kuwa Neno hudhihirishwa kwa nabii. Sasa huu hapa unabii wake umetimizwa, yeye “angemtambulisha Masihi.” Naye huyu hapa nabii na Neno, pamoja.

158 Basi akasema, “Nina haja ya kubatizwa na Wewe. Basi kwa nini Wewe waja kwangu?”

159 Yesu akamtazama moja kwa moja usoni, na kusema, “Ruhusu iwe hivyo, kwa kuwa imetupasa, inatubidi, imetupasa, kutimiza haki yote.” Basi hapo alipombatiza, angalieni, ilikuwa ni kitu gani? Yesu akasema, “Kama nabii, unajua Mimi Ndimi Dhabihu, nayo Dhabihu haina budi kuoshwa kabla haijatolewa.” Amina. Amina. Kwa hiyo, Neno humjia nabii, daima. Kikamilifu. Basi akamruhusu.

Kasema, “Hiyo ni kweli kabisa.”

160 “Imetupasa kwamba tuitimize haki yote. Mimi Ndimi Dhabihu. Sina budi kuoshwa. Ni sawa. Unahitaji kubatizwa. Amina. Lakini ruhusu iwe hivi, kwa kuwa imetupasa Mimi na wewe, kwamba tuitimize haki yote.” Haleluya!

161 Enyi wanaume na wanawake, vivyo hivyo inatupasa sisi, kama Wapentekoste walio na Ujumbe wa Mungu, kwamba tuitimize haki yote, na kumwamini Yeye. Inatupasa kuitimiza haki yote.

162 Angalieni, wakati, Nabii, ndipo Yeye akaenda moja kwa moja kwenye Neno. Waliposema, “Yesu wa Nazareti alikuwa ni Nabii, mwenye uwezo katika kutenda mbele za Mungu na watu.” Basi, kama Yeye alikuwa ni Nabii, aliyetambulishwa, basi alirejea nyuma moja kwa moja na kuyachukua maneno yale yale waliyodai kwamba ndivyo alivyo Yeye. Msilikose hili. Akachukua kile walichomwita, akalichukua Neno lililoandikwa na kujitambulisha Mwenyewe kuwa hilo, bali wangali hawakulipata. Hawakufahamu. Hata hivyo, walimwita Nabii; Naye huyu hapa, Nabii. Ndipo akaenda moja kwa moja kwenye Neno, na kulichukua Neno na kuitambulisha huduma Yake Mwenyewe.

163 Nao wakasema, “Hayo—hayo ni mahubiri mazuri, vema. Mioyo yetu iliwaka ndani yetu.” Jambo ndilo hilo. Lakini jambo ndilo hilo.

164 Sijui kama tungaliweza kufanya jambo lile lile? Imeandikwa kwamba tutalifanya, hiyo ni kweli, kwa hiyo tutalifanya. Angalieni.

165 Loo, ni ishara ya jinsi gani ya nabii wa kweli, daima moja kwa moja kwenye Neno! Ingawa, wasingeweza kulielewa. Yeye alikuwa . . . Mafundisho Yake yalikuwa ni makuu sana.

166 Na, jamani, loo, jamani, wakati huo huenda wapi? Karibu dakika nane, wakati wa kufumukana. Angalieni. Siwezi kuelewa ambapo hizo dakika arobaini na tano huenda upesi hivi.

167 Angalieni. Angalieni hapa. Ingawa wasingeweza kuelewa, ingawa labda huwezi, bali naomba ufanye yale waliyofanya. Walimwalika aingie ndani. Walisema, "Karibu. Ku—kumekuchwa. Karibu." Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. Ndipo basi, na ndipo tu, Yeye anapoweza kujitambulisha, unapomwalika kuingia ndani.

168 Unasema, "Sielewi mimi. Nimelisikia likielezewa kwa Neno, jinsi mambo haya yanavyopaswa kutukia katika siku hii, bali si—si—si—siwezi kulielewa."

169 Lakini, hata hivyo, mwalike. Sema, "Karibu, Bwana Yesu." Kwa nini usifanye hivyo sasa hivi, unaona, "Karibu"?

170 Jinsi, angalieni sasa, baada ya wao kusema. Alitenda kana kwamba angepita na kuwaacha. Huenda akafanya hivyo kwako. Bali hatapita, kama utamwalika. Yeye alisema, alienda, akaendelea, kana kwamba angeendelea mbele. Nao wakasema, "Usiku wa leo, kumekuchwa, sasa Wewe njoo ukakae pamoja nasi."

171 Kwa hiyo akageuka, kasema, "Vema, nitaingia." Kwa hiyo, akaingia ndani. Sasa, hilo ndilo jambo muhimu.

172 Ingawa usingelifahamu Neno; wewe, lina kilindi sa—sana ama chochote kile. Hulielewi. Umejaa kabisa kanuni za imani mbalimbali. Na hii ilisema vile, na hivi na vile. Na maskini nia yako, kwa hiyo hujui la kuwazia. Nitakwambia utakachofanya. Fanya tu kama walivyofanya. Sema, "Karibu, Bwana, na ukae nami usiku huu tu. Sivyo? Ingia tu na ukae pamoja nami sasa."

173 Basi anapoingia ndani, wanaufunga mlango. Angalieni jinsi alivyolifanya jambo hili sasa.

174 Angalia jinsi alivyojitambulisha kwao, baada ya Neno lililohubiriwa kushindwa, Neno lililohubiriwa na Neno lililotambulishwa. Nao walidai kwamba Yeye ni Nabii. Nao walidai kwamba ni wanafunzi Wake. Naye alisema nao, siku nzima, na bado hawakulipata kwa Neno lililohubiriwa. La, bwana. Hawakulipata. Lakini mara walipoingia, mara walipoingia ndani, Yeye aliyafumbua macho yao wapate kuona Yeye alikuwa ni Nani. Aliyafumbua macho yao.

175 Alifanyaje hilo? Kwa kufanya jambo fulani jinsi tu alivyofanya kabla ya kusulibishwa Kwake. Aliyafumbua macho yao, na kumwona akifanya jambo walilokuwa wamemwona akifanya, na Yeye—Yeye pekee hulifanya.

176 Yeye ni tofauti na watu wengine wote. Ukipata kumwona mara moja, kuna—kuna . . . Hakuna mtu anayeweza kufanya yale afanyayo. Mnaona? Wala hawalifanyi jinsi Yeye anavyolifanya. Naye daima amelifanya jinsi hiyo, wala kamwe habadiliki. Na Waebrania 13:8 ni ya kweli, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

177 Akiisha kuingia ndani, mara alipoingia ndani yao, basi alijitambulisha Mwenyewe kwa kufanya jambo ambalo Yeye . . . jinsi alivyolifanya daima.

178 Jinsi tu alivyomfanyia yule mwanamke kisimani. Angalieni. Huyo hapa anakuja, maskini mwanamke mwenye kiburi sana, mwenye sifa mbaya. Labda maskini mtoto huyo alikuwa amefukuzwa akaenda mtaani, kuishi vyovyote. Lakini papo hapo moyoni mwake alikuwa na mbegu iliyochaguliwa tangu zamani imekaa pale.

179 Na hao makuhani na kadhalika kule, walikuwa na—walikuwa na elimu, dha—dhana. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kwanza. Yeye alisema hivyo.

180 Lakini maskini mwanamke huyu, maisha yake yalikuwa yameharibika kabisa. Papa hapa chini kulikuwako na nuru kidogo, lakini huko chini kabisa kulikuwako na mbegu ikingojea. Mnaona? Na hakika kama vile nuru inavyoweza kuimulika mbegu iliyorutubishwa, itaishi.

181 Kwa hiyo, huyu hapa anakuja. Labda alikuwa amechelewa kazi yake. Asingeweza kuja pamoja na wanawake wengine, kwa vyovyote vile. Yeye, labda maskini msichana mrembo, alibeba mtungi wake wa maji mgongoni mwake. Ndipo akaenda na akaanza kuuteremsha kwenye . . . kisima. Akamsikia Mtu huyu akisema, "Nipe maji ninywe." Akaanza kuzungumza naye.

Ndipo akasema, "Nenda kamwite mume wako mje naye hapa."

182 Sasa, mnaona, chini, yeye alijua ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi. Akamwambia, "Sina mume."

183 Kasema, "Hiyo ni kweli. Umekuwa na watano. Yule uliye naye sasa siye mume wako."

184 Akasema, "Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Hatujakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Ninaona kwamba Wewe ni nabii. Sasa, tunajua ya kwamba tunamtazamia Kristo, Masihi mpakwa mafuta. Naye ajapo, hivyo ndivyo atakavyokuwa hasa."

Sasa angalieni. Yeye alisema, "Mimi Ndiye, ninayesema nawe."

185 Moja kwa moja akaenda mjini. Hakuwa na haki ya kufanya hivyo, kulingana na torati zao. Mwanamke wa namna hiyo, mwanamume asingalimsikiliza. Lakini ati ujaribu kumkomesha? Kama nyumba inayoungua moto, kwenye siku

yenye upepo. Huyu hapa anaenda. Akasema, "Njoni, mmwone Mtu ambaye ameniambia mambo ambayo nimefanya. Yamkini kuwa Huyu Ndiye Masihi?"

186 Sasa kumbukeni, Yesu kamwe hakulirudia. Kamwe hakufanya wakati mmoja mle ndani, bali walisema mji mzima ulimwamini kwa sababu ya ushuhuda wa mwanamke huyo. Wazia hilo. Loo, jamani!

187 Wakati alipojua ile ahadi, kile Masihi angekuwa, na wakati alipoiona ahadi hiyo imetimizwa, iliyafumbua macho yake. Mnaona? Yalikuwa yamefungwa kwa dhambi, bali wakati ahadi hiyo . . . Alisema, "Hiyo . . . Masihi atafanya hivyo atakapokuja."

188 Akasema, "Mimi Ndiye." Macho yake yakafumbuliwa. Ana Uzima wa Milele kwa kuwa macho yake yalifumbuliwa.

189 Macho ya Petro yalifumbuliwa; ya Nathanaeli. Tulizungumza juu yake jana usiku.

190 Limefanya nini kwa macho yetu katika siku hizi? Ahadi iliyotimizwa, je! imeyafumbua macho yao? Tumeona katika Yohana 14:12, Waebrania 13:8, Yohana Mtakatifu 14:9, na tumeona Luka 17:27-28, na Maandiko haya yote yaliyoahidiwa, Malaki 4, yote yametimizwa papa hapa mbele zetu, je! hiyo imefanya nini kwa macho yetu? Isipoyafumbua, itayapofusha Milele. Huyafumbua mengine, ikayapofusha hayo mengine. Mnaona? Huyafumbua ya wale inaninii . . . siku hizi za mwisho, kile alichoahidi kufanya. Hivi ndivyo Yeye alivyosema, angefanya hivyo, "Kuirudisha ile Imani."

191 Loo, enyi Wapentekoste, wenye kumkiri Roho Mtakatifu wa Mungu, Mungu wa Mbinguni na afumbue—ayafumbue macho yenu kutokana na mapokeo, yamwone Mungu aliye hai, kwa ahadi ya Biblia tunayodai tunaiamini, kile alichosema Yeye atafanya. Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, ulioitwa katika siku ya mwisho, Naye Yehova angeshuka miongoni mwa miili ya watu Wake na kufanya vile alivyofanya hasa katika siku za Sodoma.

192 Je! mlisikia habari usiku wa leo, jinsi ambavyo, katika mkoa uu huu, ninasahau ni mamia mangapi ya walimu, walimu wa shule, walithibitishwa kwamba ni walawiti. Habari za usiku wa leo. Loo, imeoza mpaka mashinani, kila kitu. Serikali, wanadai, na wafanyakazi wa serikali, kuna karibu asilimia arobaini yao, imethibitishwa, ni walawiti. Ofisi yangu imejaa barua, mama akilia, kwamba mvulana wao anaishi na wavulana. Na, mnaona, ni ile siku tu tunayoishi. Kila kitu!

193 Mataifa yanavunjika. Israeli inaamka. Wako kwenye nchi ya wenyeji wao. Mtini unachipusha majani yake.

194 Loo, kanisa limelala katika Laodikia. Naye Yesu, akijaribu kupata ushirikiano, wala hata hawezi kuupata! . . . ? . . . Mnaona? Hata hivyo, pamoja na mambo yote ambayo Maandiko

yanasema, kanisa linasinzia moja kwa moja, katika kitanda cha kilimwengu.

195 Loo, kanisa, kama hamwezi kulifahamu Neno, fungueni tu moyo wenu mwone ikiwa Yeye hajitambulishi kama alivyofanya wakati huo, "yeye yule jana, leo, na hata milele."

Na tuviinamishe vichwa vyetu kwa kitambo kidogo.

196 Baba wa Mbinguni, wakati mwingine labda...Sitaki kuwakemea watu. Simaanishi kuwa mkali. Lakini, Bwana, ni matamshi ya seremala, "Unawezaje kuufanya ubao ushike, usipoupigilia msumari?" Kwa hiyo naomba, Mungu, kwamba wataelewa ya kwamba ni kupitia tu kwa upendo wa Kikristo ambapo—ambapo tunajaribu kulishindilia Hili. Huenda ikawa ni kuzuriwa kwa baadhi ya watu hapa, kwa mara ya mwisho ambapo watapata kuruhusiwa. Huenda ikawa ndiyo mara ya mwisho tutakapokutana kamwe. Huenda mji huu usipate uamsho mwingine kama huu.

197 Hata hivyo, pana siku, wataendelea, "kuwa na uamsho," wanadai, nalo kanisa tayari limeondoka, limetiwa muhuri tayari, mlango. Nuhu alikuwa katika safina wakati mlango ulipofungwa nyuma yake, siku saba kabla mvua haijapata kuja, hata hakuna mtu angaliweza kuingia kwenye safina. Ulimwengu uliendelea moja kwa moja, vivyo hivyo tu.

198 Na siku moja huenda ikawa ni jambo lile lile, huenda wakaamkia yale Yesu aliyosema, wakati wanafunzi waliposema, "Kwa nini waandishi husema, 'Eliya hana budi kuja kwanza'?" Yesu akasema, "Amekuja tayari wala hamkujua."

199 Ndivyo ingeweza kuwa, kule Kuja, na kunyakuliwa. Moja ya siku hizi, wataingia kwenye ile Dhiki. Watasema, "Nilifikiri Bibi-arusi alikuwa aondoke. Je! kanisa linaingia kwenye ile dhiki?" Hakika, kanisa litaingia kwenye ile dhiki, bali sio Bibi-arusi. "Kwa nini hili linapaswa kutukia kwanza?"

200 Ndipo Neno huenda likawa, "Limeondoka tayari. Hamkujua." Wataendelea, kuwa na kanisa, kama kawaida.

201 Mungu, wajalie watu, usiku wa leo, ingawa hawayaelewi Maandiko, huenda yakawa ni fumbo kwao, bali jalia tu kila mmoja aseme, "Basi, Bwana Yesu, Wewe uliyepo, karibu ukae nami. Ni—nina haja. Nilisoma katika Biblia ambapo mwanamke aliligusa vazi Lako, na Wewe ukageuka na kumwambia shida yake ilikuwa ni nini, na ukasema ya kwamba imani yake ilimwokoa. Nami ninasoma haya katika Biblia, ya kwamba wewe sasa ni 'kuhani mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu,' na Wewe ni 'yeye yule jana, leo, na hata milele.' Sasa ingia moyoni mwangu, Bwana, na unifunulie. Ingawa nimetembea, na nimekupenda, bali kwa kweli sijapata kuliona likifanywa. Kwa hiyo naomba, Mungu, kwamba utanifanyia hilo, usiku wa leo."

202 Wajalie watu hao, Baba. Na jalia macho yetu yafumbuliwe, kote kanisani, nasi tutamwona huyo Bwana Yesu mpendwa, mwema, aliyefufuka, yeye yule jana, leo, na hata milele. Tujalie. Jalia macho yetu yafumbuliwe, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

203 Sasa, kuwaacha mfumukane katika wakati mzuri, nisingekuwa na wakati wa kufanya mstari wa maombi hapa juu, ingawa labda walipewa kadi za maombi. Haiwabidi kuwa hapa juu. Mungu ni mkuu jinsi ile ile, huku nje, kama alivyo mahali popote.

204 Yeye, mnafikiri, anaenea kila mahali? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika, Ndivyo alivyo. Yeye anaenea kila mahali kwa kuwa anajua yote. Sasa, Yeye anarudi tena, maana Yeye, kwa kuwa mjua yote, anajua mambo yote. Kwa hiyo, basi, Yeye—Yeye yuko kila mahali, kwa kujua yote.

205 Ni kama tu neno kuchaguliwa tangu zamani, ni neno baya. Nililitumia dakika chache zilizopita, nami nikajishika, maana nilihisi roho ikirudi nyuma. Watu wengi hawaamini katika kuchaguliwa tangu zamani. Kuchaguliwa tangu zamani ni Neno baya. Kwa kweli ni kutangulia kujua. Mungu anajua, awali, ni nani atakayekuwako na ni nani hatakuwako, kwa hiyo basi anaweza kuchagua kwa kutangulia Kwake kujua. Hiyo ndiyo sababu Yeye anajua ni nani atakayekuwako na ni nani hatakuwako. Mnaona? Haninii... Yeye, "Hapendi mtu yeyote apotee." Bali anajua yule atakayepotea. Kama hakujua, basi Yeye hakuwa ni Mungu. Inampasa kuwa mwenye nguvu zote kama vile—vile anavyoenea kila mahali; mnaona, mjua yote, aliye kila mahali, mwenye nguvu zote, asiye na kikomo. Hana kikomo. Kama sivyo, Yeye si Mungu. Kwa hiyo anajua mambo yote, basi anaweza kujua mwisho tangu mwanzo, kwa kuwa Yeye ni Neno.

206 Sasa, mimi ni mgeni kabisa. Sioni mtu hapa nimjuaye, isipokuwa iwe ni mvulana huyu papa hapa. Kama ninamjua mvulana huyu, hivi hukuwa na ndevu kubwa ama kitu kama hicho, uliyokuwa nayo, muda mrefu uliopita? Kwa namna fulani nilikwambia habari zake, wakati na—nafikiri wewe ndiye, jamaa hawa wanaoketi hapa mbele. Nje ya huyo, sioni mtu nimjuaye. Siwezi kumwona mmoja huko. Imetokea kwamba nilitazama tu. Mvulana huyo aliketi pale, akilia, dakika chache zilizopita, akiyapangusa macho yake. Nikawazia, "Yule anaonekana kama jamaa yule yule niliyekuwa na mahojiano ya faragha naye wakati mmoja." Hata sijui ametoka wapi. Niliutambua tu uso wake. Sijaninii... Mnaona? Lakini huyo ndiye mtu tu ninayemjua humu ndani sasa. Vema.

207 Sasa je! utafungua tu moyo wako namna hii? Ni wangapi wenu wanaomhitaji Mungu? Inua mkono wako, useme, "Mimi ni

mhitaji. Nina haja.” Sijui tu kuwa wewe ni nani. Inua tu mkono wako. Nami niliona.

208 Sasa Mungu wa Mbinguni, ambaye alimfufua Mwanawe, Yesu Kristo, ambaye kwa Neno Lake lililoandikwa ninajaribu, kwa karama ya Kiungu, kuutambulisha Uwepo Wake mbele ya watu hawa, kwa ajili ya utukufu wao, na amtume Roho Mtakatifu juu yangu. Wakati, kwa karama hii, ninajiachilia, kuninii. . . kumtambulisha Yesu Kristo katika mwili wa kibinadamu, kama vile Mungu alivyotambulishwa katika mwili wa kibinadamu katika siku za Sodoma, kuzitimiza kazi Zake. Na alijalie katika Jina la Yesu Kristo.

209 Sasa kwa uchaji, kila mtu, sasa anza tu kuomba moyoni mwako, “Bwana Yesu, nitaufungua moyo wangu. Nawe karibu. Na jalia nifungie mbali kutokuamini kwangu kwote, nje. Kisha unijulishe, jambo ulilofanya kabla ya kusulibishwa Kwako, ndipo nitajua kuwa Wewe umefufuka katika wafu.”

210 Sasa haiwezi kushika kila mmoja wenu. Hiyo ni kweli kabisa. Lakini baadhi yenu, hapana shaka, hao itawashika. Na kama ikimshika mmoja, kama tu vile yule mwanamke huko nje, wengine wetu (watu waliokuwa Sikari) haikubidi hilo litendwe kwao. Waliamini. Na ikiwa mtu fulani, mwanamke mmoja tu, mwanamume mmoja, mvulana mmoja, mtoto mmoja, yeyote yule, angetambulishwa jinsi hiyo; kama hao watu huko nyuma, ambao hawajapata kumwona Yeye, nasi tumefundishwa hivyo, hakika inatupasa kuamini. Hiyo ni kweli, ndugu? Hilo linaonekana la busara kwenu? [Wahudumu wanasema, “Amina.”—Mh.] Hakika.

211 Ni vigumu wakati unahubiri namna hiyo, kisha unakuja . . . Mnaona, ni karama mbili mbalimbali. Moja ni kuzungumza; hiyo nyingine ni kuona.

212 Sasa amini tu kwa moyo wako wote. Usitilie shaka. Usitilie shaka. Kuwa tu na imani kwa Mungu. Hebu tuanze kuangalia upande huu *hapa* mahali fulani. Mtu fulani na aangalie tu. Itakubidi kusimama pale, namna zote za imani. Usilisukume; unaona, utaruka juu yake. Ndivyo ilivyo. Ni kama tu sehemu yako. Unaona? Jilegeze tu, na kusema, “Vema, hakika, hilo ni Neno. Ninaliamini. Maskini jamaa yule mdogo pale juu, hanijui. Lakini ninamjua Yesu. Amesema kweli juu ya Neno, nami ninaliamini.” Fanya tu hivyo, useme, “Mimi ni mgonjwa na mhitaji, na nina haja.” Siwezi kukuponya, wala hii haiponyi, bali inatambulisha tu.

213 Si ajabu ninyi watu mnaweza kushuku. Mna—mnaona tu mguso Wake mmoja hapa. Inasema kile kitakachotukia, na ni nani, wapi, na yote kulihusu. Wala hakuna hata wakati mmoja, kamwe haijashindwa hata wakati mmoja, katika makumi elfu ya nyakati, kote ulimwenguni. Ni wangapi wameifuata, na wanajua ni Kweli. Inua mkono wako. [Kusanyiko linasema, “Amina.”—

Mh.] Mnaona? Vema, jamani! Mnaona? Kamwe . . . Hiyo, haiwezi kuwa ni kitu kingine ila Mungu, na kuwa sahihi jinsi hiyo, mnaona, kwa maana ni ahadi Yake. Kamwe haiwezi kushindwa. Sasa, Yeye haninii . . .

214 Hiyo haikuponyi, maana Yeye tayari amekuponya. Yeye anatambulisha tu yupo hapa kutimiza ahadi hiyo. Sasa, kama ameitimiza ahadi hiyo, Yeye huitimza ahadi ya uponyaji. Hiyo ni kweli, ndugu zangu? [Wahudumu wanasema, "Amina."—Mh.] Yeye huitimiza ahadi Yake ya uponyaji kama hutimiza ahadi hiyo. Ni ishara ya hakika zaidi.

215 Vipi kama mtu alikuwa hapa katika kiti cha magurudumu, nami nikawachukua, kingekuwa ni kisa kizuri cha saikolojia, ama maskini kitu fulani kingaliweza kumfanya mtu huyo kutembea. Bali hakiwezi kuyatambua mawazo ya moyo. Mnaona? Hilo ni jambo moja la hakika. Kujua yale uliyofanya, kwamba wewe ni nani, na yote kukuhusu, hilo linamhitaji Mungu, pekee, kuwa kamilifu kila wakati.

216 Hapa, la—laiti—laiti ningaliweza kuelezea jambo hili. Hakuna haja ya mimi kujaribu kulielezea. Usingeweza kulielezea.

217 Lakini sasa, kama ningaliweza kusema neno hili, kitu fulani ndani yangu kilichobadilika kikaingia katika kiwango kingine. Mnaona? Ninaangalia moja kwa moja kwenye ile Nguzo ya Moto iliyowafuata Israeli nyikani. Ni wangapi waliopata kuiona picha Yake? Hebu tuone mkono wako. Hakika. Ninaiangalia moja kwa moja, papa hapa, ninaiangalia moja kwa moja, kaharabu, kidogo inaonekana ya kimanjano na chanikiwiti, ikizungukazunguka.

218 Ninamwona mwanamke akisogea. Ameketi papa hapa, naam, akiniangalia moja kwa moja. Naye ameketi papa hapa chini, akiniangalia moja kwa moja. Naye huugua. Yeye anauombea ugonjwa alio nao. Ni ugonjwa wa damu. Ni kisukari. Hiyo ni kweli. Hiyo ni ninyi wawili. Ninyi wavulana wawili wadogo mnaoketi hapo, mkiniangalia, mna kisukari. Mnaona?

219 Sasa, ni kitu gani hicho? Ulikuwa ukiwazia hilo, sivyo, ukijaribu kuufungua moyo wako? Nilikuona ukiingia moja kwa moja. Imefanya jinsi alivyofanya hasa kabla ya kusulibishwa Kwake. Sasa, hunijui mimi, sivyo? Hakuna mmoja wenu anayenijua. Kama hiyo ni kweli, inueni mikono yenu, ikiwa hamnijui. Vema. Vema. Hamnijui. Basi, ilibidi iwe ni Yeye, maana siwajui mimi. Ilibidi iwe ni Yeye.

220 Kama tu utaamini, kwa moyo wako wote, Mungu atalidhihirisha. Inakubidi uamini hata hivyo.

221 Hapa, kuna mtu aliyenong'oneza, akasema jambo fulani kwa mtu fulani. Ameketi papa hapa akiniangalia, kidogo ni mnene, amevaa shati jeupe. Hatufahamiani, bwana. Hiyo ni kweli? Ameketi papo hapo karibu nawe. Je! ninakujua? La. Iko nyuma yako, bwana. La, nyuma yako. Huyo mtu aliye na

shati jeupe. Tulia tu. Wewe, wewe amini. Mtu mwenye shati jeupe. Kama Mungu. . . Huyo ni wewe. Naam. Uliangalia huku na huku. Kama Mungu ataniambia shida yako ni ipi, utaamini atauponya? Una matatizo ya moyo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Unaukubali uponyaji wako?

222 Sasa, kuna mtu huku, aliuinua mkono Wake, mahali fulani hapa. Iko kwenye maskini ninii hii. . . Wewe, je! unaamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu, nabii Wake? Unaamini? Wewe pia unaugua ugonjwa wa moyo. Una yabisi kavu, pia. Huyo ni mke wako aliyeketi karibu na wewe, naye anaugua yabisi kavu. Na pia ana vipindi vya mpagao. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Unaamini ninaweza kuwaambia ninyi ni akina nani? Bw. na Bibi Jones, mnaweza kuamini, amininі sasa mpate kuponywa.

223 Amini kwa moyo wako wote. Hatufahamiani nawe. Mwamini Mungu. Usitie shaka. Amini tu.

224 Huyu hapa mtu ameketi, kidogo ana mvi, ameketi papa hapa mwishoni, huchana nywele yake, upande mmoja. Hiyo hapo ile Nuru imesimama karibu nawe, bwana! . . . ? . . . Unaamini mimi ni nabii wa Mungu, mtumishi Wake? Unaamini hayo mafua yaletwayo na vumbi yatakuacha, nawe utakuwa mzima? Unaamini? Inua mkono wako. Sasa, hatufahamiani kabisa. Hilo ndilo ulilomb ea.

225 Mtu anayefuata, yeye aliuinua mkono wake, pia, kwa sababu aliamini. Vema, nini. . . Yeye hana mafua yaletwayo na vumbi, bali ana yabisi kavu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Punga mkono wako, bwana. Hiyo ni kweli. Sasa, unaamini? Mungu atampa neema hiyo, kuwa na imani.

226 Maskini mama huyu anayeketi papa hapa mwishoni. Je! unaamini, mama, unaamini kwa moyo wako wote? A-ha. Unaamini kwamba matatizo hayo ya tumbo yatakuondokea? Unaamini? Una mzigo moyoni mwako, sivyo? Huo ni kwa ajili ya binti yako. Hayupo hapa. Unaamini kwamba nikwambie mahali anapoishi? Anaishi Kalifornia. Ana uvuli mweusi juu yake. Atakufa kama hatashughulikiwa, kwa maana ametiwa uvuli na kansa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Unaamini ninaweza kukwambia wewe ni nani, kwa msaada wa Mungu? Yesu alimwambia Simoni kwamba alikuwa ni nani. Hiyo ni kweli? Bibi Ackerman. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako. A-ha. Kweli.

227 Maskini mama mmishenari aliyeketi hapo karibu nawe, kidogo anahofia mambo fulani, pia. Hiyo ni kweli. Anamwombea rafiki, umedhoofika sana, wewe mwenyewe. Hiyo ni kweli? Nawe ni mmishenari? Amini kwa moyo wako wote. Sikujui, kamwe sijawahi kukuona. Lakini hiyo ni kweli.

228 Huyo mama anayeketi nyuma yako, mwenye mvi, anayeumwa na tumbo. Unaamini kwamba Mungu atakuponya huo? Unao huo, pia.

229 Mnaamini kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Ni kitu gani? Ni kutambulishwa. Sasa, Neno lilisema hivyo, sasa Huyu hapa akiingia mioyoni mwenu na kujifunua Mwenyewe kama tu alivyofanya. Je! hayo si ni yale hasa aliyofanya kabla ya kusulibishwa Kwake? Inua mkono wako. Basi, Yeye amefufuka katika wafu. Mnaamini hilo? ["Amina."] Na sasa ikiwa mko katika Uwepo Wake wa Kiungu, je! macho yenu yamefumbuliwa kutambua ya kwamba Mungu yeye yule mtakayesimama mbele Zake kwenye Siku ya Hukumu, yupo papa hapa miongoni mwenu sasa? Naye anajua kila kitu mtakachowazia.

Waweza kuinamisha kichwa chako sasa?

230 Je! unawaza juu Yake? Ungetaka awe Mwokozi wako? Ikiwa unataka, waweza kusimama kwa ajili ya maombi? Wewe unayetaka awe Mwokozi wako, tusimame tu kwa maombi. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Angalia tu. Sasa, tusimame tu, dakika moja, nipate kuwaombea. Simama. "Ninataka kumkubali kama Mwokozi wangu. Katika Uwepo wa Kiungu wa Utu Wake sasa, ninataka kumkubali kama Mwokozi wangu." Kungekuwako na wengine zaidi? Ninaamini hivyo, kwa hiyo naomba msimame tu kwa miguu yenu. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

231 Fanya hivyo sasa, unaona. Usingoje mpaka kesho. Kesho huenda ikachelewa sana. Leo hii Yeye ni Mwokozi wako, kesho huenda akawa Hakimu wako. Unaona? Kwa hiyo sasa, kama ananena na moyo wako, kama vile tu ulivyoufungua moyo wako. Mungu akubariki, wewe. Hiyo ni kweli. Endeleeni tu kusimama. Kama unaamini kwa moyo wako wote, je! utamkubali, wakati ukiwa Mbele Zake? Utamkubali? Ungefanya hivyo? Ungemkubali tu kama Mwokozi wako?

232 Sijui, kama utafanya hivyo, wakati ukiweka mkono wako juu ya moyo wako, namna hii, kila mmoja wenu. Na tuombe. Sasa wewe omba kwa njia yako mwenyewe, "Mungu, unirehemu, mwenye dhambi."

233 Halafu mnapofanya hivyo, ninawatakeni, katika dakika chache, mje hapa juu na kushuhudia ya kwamba mmemkubali kama Mwokozi wenu. "Kwa maana kama m—mtanishuhudia mbele za watu, huyo nitamshuhudia mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu. Ukinionea haya mbele za watu, huyo nitamwonea haya mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu." Sasa angalia, kumbuka, Yeye anaujua moyo wako. Amethibitisha hilo. Yeye ni Neno. Sasa nawetakeni mfanye hivyo, katika dakika chache.

Niwatakeni ninyi, sasa, mumkubali, tunapoomba.

234 Bwana Yesu, wakati ile Nuru ilipokuwa ikisonga, waliko watu, maono yalikuwa yakitokea juu ya watu. Mara, inakoma. Na nikirudi, Wewe uliniambia nifanye hivi. "Kutii ni bora kuliko dhabihu."

235 Na, Bwana Yesu, kwenye ku—kundi hili la watu, wengi wao wanakuamini sasa hivi. Wanakukubali Wewe kama—kama Mwokozi wao. Wanaamini. Wanajua kwamba ni kweli. Walikuwa papa hapa wakati lilipotukia, nao wanajua ya kwamba Wewe umefufuka katika wafu, na ungali hai, na wanajua kwamba tunaelekea Hukumuni, kukutana na Wewe kwenye Kiti cha Hukumu cha Kristo. Nasi tunataka msamaha, Bwana. Wewe ulisema, katika Neno Lako Mwenyewe. Nitalinukuu, Baba, kusudi tu kwamba—kwamba tujue. Ulisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu," hayo ndiyo tumekuwa tukinena hasa usiku wa leo, "na kumwamini Yeye aliyenipeleka," wanamwamini, "yuna," wakati uliopo, "Uzima wa milele wala kamwe hataingia Hukumuni, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani." Sasa, hilo ni Neno Lako, Bwana, kama tu vile Yohana 3:16 na Neno lingine lote. Wewe ulisema, "Yeye atakayeamini."

236 "Yeye atakayenikiri Mimi," tena, Yeye alisema, "mbele za watu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu. Lakini kila atakayenionea haya mbele za watu, huyo nitamwonea haya mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu."

237 Sasa, popote katika Uwepo wa Kiungu, ulivyokuja usiku wa leo, nasi sote tupo hapa, waaminio Wakristo, tunauhisi Uwepo wa Utu Wako mkuu, ile hisi nzuri sana tukufu ya Kiungu, ama Mungu akitembea huku, miongoni mwetu. Si ajabu, Bwana, inayapofusha macho ya asiyeamini ambaye haliamini Neno. Na jinsi inavyoyafumbua macho ya hao watakaoamini!

238 Sasa, Wewe umeyafumbua macho ya watu hawa, kwa kujifunua Mwenyewe kwao. Sasa, Bwana, yafumbue macho ya watu hawa na ufanye maskani Yako pamoja nao, Baba. Wao ni Wako. Ninawakabidhi Kwako. Hao ni nyara za Neno Lako. Neno Lako limewaita, nalo Neno Lako limewatambulishia. Na sasa wamejitambulisha, kwa kusimama wapate kutoa ushuhuda kwamba wanataka uwasamehe dhambi zao. Ulisema, "Yeye anijiaye Mimi, sitamtupa nje kamwe." Na mbingu na nchi zitapita, bali Neno Lako halitashindwa. Hao ni Wako, Bwana. Ni mali Yako. Katika Jina la Yesu Kristo, ninamdai kila mmoja. Nalo Jina Lako litasifiwa kwa ajili yake.

239 Jalia wahesabiwe katika Bibi-arusi, waingie kwenye ufufuo. Kama nisipopata kuwazungumzia, juu ya nchi, ama kupeana mikono nao, na majaliwa ya kuwabatiza katika ubatizo wa Kikristo, naomba, Mungu, kwenye Siku ile wakati yote yamekwisha na tumeketi kwenye Karamu ya Arusi, naomba

nipate majaliwa, niangalie upande wa pili wa meza. Waseme, "Loo, mbona, ilikuwa huko Tampa, Florida, usiku ule, Ndugu Branham, ambako nilisimama." Niseme, "Sasa Huyu hapa. Unaona, ni Yeye yule." Tujalie, Bwana. Wadumishe kwa neema Yako. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

Basi mwaweza kuketi.

240 Dakika chache tu, tutawaalika mje huku juu na kulitambulisha jaribio lenu.

241 Sasa, ninyi mliosimama kwa miguu yenu, ninyi mliosimama wakati maombi yalipokuwa yakiendelea, mlishuhudia kitu fulani, kwamba mmefanya haki, nanyi mnaamini Yeye ni Mwana wa Mungu, na sasa mnamkubali kama Mwokozi wenu binafsi? Inua mkono wako, useme, "Sasa ninamkubali." Mungu awabariki. Inaonekana kana kwamba ni asilimia mia moja. "Sasa nimemkubali kama Mwokozi wangu."

242 Sasa hatua yako ya pili ni kujazwa na Roho Mtakatifu. Mna chumba cha hilo, sivyo, ndugu, chumba cha hilo hapa? Naam, bwana. Watakushauri zaidi ndani ya hicho.

243 Sasa, kuumalizia mstari wa maombi, hebu. . . Sasa, msiwe mkienda huku na huku. Mnaona, kila unaposogea, hilo linamkatiza Roho wa Mungu. Mnaona? Sasa msisogee. Mimi hapa, nimechelewa tena. Wekeaneni mikono, na mwekeleane mikono tu na kuombeana. Sasa jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. Kila mmoja wenu ni waaminio.

244 Loo, naam, hivi hamjisikii vizuri? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Je! hamjisikii kana kwamba sasa mko Mbele za Mungu, ile hisi tamu, nyenyekevu? Nafsi zetu na zisichukuliwe sana jinsi hiyo na ulimwengu na kadhalika. Wakati, ile hisi tamu ya kupendeza ya Masihi wetu mkuu, Yesu Kristo, ikiwa moja kwa moja miongoni mwetu sasa katika umbo la Roho Mtakatifu. Ulimwengu haujui kitu kuihusu. Bali sisi tunamjua. Tumemwona. Tumemwona akijitambulisha Mwenywe.

245 Kumbukeni, katika siku za Ibrahimu, kwamba—kwamba Mungu aliyekuwa katika mwili wa kibinadamu, kamwe hakushuka kwenda huko Sodoma. Kulikuwako na wahubiri wawili walioshuka kwenda huko, bali si Yeye. Yeye alikaa pamoja na Kanisa teule, lililoitwa litoke. Hao ndio Ujumbe Wake ulielekezewa. Si ni ajabu kwamba Yeye huja kwetu, leo hii? Tunajiona wenyewe tumetambulishwa kama Uzao wa kifalme wa Ibrahimu. Ambaye, huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema, alisema yale Sara aliyokuwa akiwazia. Kitu hicho hicho kinakuja moja kwa moja hapa usiku wa leo, kinafanya jambo lile lile, katika mwili wa kibinadamu. Yesu alisema ingetendeka, "Siku ambapo Mwana wa Adamu alifunuliwa."

246 Sasa, Yeye alisema jambo hili lingine, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

247 Sasa huku mmeshikana mikono, mioyo yenu pamoja, na tuinamishe vichwa vyetu sasa na kuwaombea wagonjwa.

248 Baba yetu wa Mbinguni, mwenye rehema, tunakuletea wasikilizaji hawa wanaongojea, na wakiwa kwenye Uwepo huu wa Kiungu, Ee Mungu. Si ajabu hao wanafunzi, Kleopa na rafiki yake, iliwachukua siku nzima kufika Emau. Lakini, dakika chache, walikuwa wamerudi. Walikuwa pamoja na hao wanafunzi wengine. Hawakuja kubishania misimamo yao ya kidini, bali walikuja kwa sababu walikuwa wamemwona. Walikuwa katika...Walikuwa wamekutana na Yeye. Wa—walimsikia akihubiri, na wakamwona akijitambulisha, kwamba alikuwa ni Kristo aliyefufuka.

249 Wewe ni Neno. Neno limehubiriwa. Neno limedhihirishwa. "Ne—Neno huyatambua mawazo yaliyo moyoni." Linasema hivyo. Nasi tuna hakika kama walivyo wao, Bwana, hakika tu kama walivyokuwa. Tunaiona ishara ya ufufuo, nasi tunajua ni utambulisho Wako ukijifunua Mwenyewe, kwa kuwa Kanisa Lako na Neno hawana budi kuwa ni kitu kimoja, kwa sababu mume na mke ni mmoja. Bibi-arusi na Neno wanakuwa mmoja.

250 Ee Mungu, tunapoiona miongoni mwetu, jinsi tunavyoifurahia; na kuona sifa zile zile, picha ile ile ikipigwa, kisayansi.

251 Malaika wa Bwana, ambaye aliwatoa Israeli kutoka Misri na kuwapeleka kwenye nchi ya ahadi, "alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu," akapaa Juu. Akasema, "Nimetoka kwa Mungu, narudi kwa Mungu."

252 Miezi michache baadaye, Huyu hapa kwenye njia ya kwenda Dameski, pamoja na Sauli, aliyembwaga chini. Naye Sauli, akiiona Nguzo ile ile ya Moto, alisema, "Bwana, U Nani Wewe?"

253 Akasema, "Mimi ni Yesu. Ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo."

254 Ee Bwana, kuona, miaka elfu mbili baadaye, Huyu hapa, amethibitishwa kisayansi, na kuthibitishwa kwa imani, kanisani, na kufanya jambo lile lile alilofanya, kuyatambulisha Maandiko ya leo hii kimamilifu. Hatukosi kuamini tena, Bwana. Tunaamini. Saidia kutokuamini kwetu. Jalia mioyo yetu ifunguliwe.

255 Jalia maradhi yapoteze nguvu zake. Hawa waaminio wamewekeana mikono. Maombi ya imani yanafanywa sasa hivi. "Yatamwokoa mgonjwa huyo, Naye Mungu atawainua."

256 Shetani, waachilie wasikilizaji hawa. Katika Jina la Yesu Kristo, waachilie waondoke, wapate kuwa huru na maradhi na magonjwa, kwa utukufu wa Mungu.

257 Sasa endeleeni kujifungia ndani. Anzeni tu kuomba. Omba kwa njia yako mwenyewe. Wekeaneni mikono sasa. Endeleeni tu kuomba, mseme, "Bwana Mungu," katika njia yako mwenyewe sasa. Niliwaombea, sasa ninyi ombeaneni. Iweke mikono yako juu ya jirani yako hapo, useme, "Bwana, mponye mwanamke huyu. Mponye mwanamume huyu. Ninaamini. Ninaudai kwa ajili yao. Wanaudai kwa ajili yangu. Ninaamini ya kwamba Wewe upo hapa." Mbona, ingekuwa ni kufa ganzi, kutokuamini hilo. Amini, kwa moyo wako wote.

258 Bwana Mungu na amponye kila mmoja wenu! Endeleeni tu kuomba, na kuamini. Bwana na amponye kila mmoja wenu, tangu nyayo za miguu yako hadi utosi wa kichwa chako. Amina.

Basi Macho Yao Yalipofumbuliwa, Walimtambua SWA64-0416
(And When Their Eyes Were Opened, They Knew Him)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 16 Aprili, 1964, kwenye Ukumbi wa McKay, huko Tampa, Florida, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha Ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na umechapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org